
**MWANAFUNZI** wa darasa la nne ajinyonga kwa kamba nyumbani kwao

UKURASA 4



**ANAYETUHUMIWA** kubaka mtoto wa miaka 10 Zanzibar anusurika kifo

UKURASA 17


Jumatatu Juni 14, 2021 Nipashe 11

TOLEO MAALUM

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Bajeti Nishati yaainisha mafanikio lukuki sekta ya umeme**

• Watanzania milioni 47 sasa waunganishwa na umeme

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Juni 14, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580611

www.ippmedia.com



The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710


# Samia ashtukia upigaji mabilioni

**NI** ujenzi wa jengo la Benki Kuu, aliweka kiporo sakata... *Endelea Ukurasa wa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan akivuta utepe na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Profesa Florens Luoga, kufungua jengo la ofisi ya Benki Kuu tawi la Mwanza katika sherehe zilizofanyika jijini Mwanza jana. **PICHA: IKULU**

## Wasomi wanavyomlilia Prof. Mwesiga Baregu

UKURASA 3

## NI WIKI YA KUIJADILI BAJETI BUNGENI

UKURASA 2

**MICHEZO** **MOROCCO APIGIA HESABU POINTI 12 NAMUNGO FC** UK. 23

**MAONI, KATUNI UK. 6**



Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Regina Hess, akizungumza na Rais wa Mahakama ya Afrika inayoshughulikia Haki za Binadamu, Jaji Imani Aboud, alipomtembelea ofisini kwake jijini Arusha, mwishoni mwa wiki. **PICHA: HISANI YA MAHAKAMA YA AFRIKA**

# Samia ashtukia gharama jengo la BoT

**Na Richard Makore,** MWANZA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameonyesha kutoridhishwa na gharama zaidi ya Sh. bilioni 41 zilizotumika kujenga jengo lenye ghorofa tano la Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Kanda ya Mwanza.

Ujenzi wa jengo hilo umegharimu Sh. bilioni 23.37 na uwekeji ya mitambo ya kiusalama wa benki umechukua Sh. bilioni 18.73.

"Gharama kidogo za ujenzi huu zinasisimua mishipa ya damu, lakini kwa kuwa leo ni siku ya sherehe niliache hili, lakini huko mbeleni tutashikana," alisema jana jijini hapo.

Akizungumza katika sherehe za ufunguzi wa jengo la benki hiyo, Samia alianza kuonyesha wasiwasi wake kuhusu gharama za ujenzi.

Rais Samia alisema kwa kuwa jana ilikuwa ni sherehe hatalizungumzia hilo na kwamba huko mbeleni watashikana.

Baada ya kauli hiyo, Rais Samia hakuzungumzia sakata hilo, badala yake aliendelea na hotuba yake kwa kuzungumzia mambo mengine.

**HALI YA UCHUMI**

Rais Samia akizungumzia uchumi wa nchi, alisema kwa mwaka jana ulikua kwa asilimia 4.8, licha ya kuwapo changamoto za ugonjwa wa corona, na kwamba mfumuko wa bei kwa kipindi cha miaka mitano umebaki kuwa asilimia 4.2.

Aliisifu BoT kwa kuendelea kuandaa sera mbalimbali za kukuza uchumi pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei.

Alisema BoT imefanya kazi kubwa katika kuhakikisha uchumi wa nchi unakua, huku akisema serikali kwa sasa ina akiba ya kutosha ya fedha za nje kwa ajili ya kufanya manunuzi mbalimbali ya vitu.

**RIBA ZA BENKI**

Akizungumzia tatizo la riba kubwa zinazotozwa na benki mbalimbali kwa wananchi, Rais alitaka ishuke hadi kufikia chini ya asimilia 10.

Alisema hakuna sababu ya benki za biashara kuendelea kutoza riba ya asilimia 12 hadi 19, na kwamba kama kuna matatizo ya mifumo ishughulikiwe haraka.

Aliongeza kuwa kuna taasisi za fedha ambazo zilikuwa zinakopesha riba kubwa zaidi, na kwamba baada ya kuona tatizo hilo serikali iliamua kutunga sera, sheria na kanuni ili kuondoa tatizo hilo.

Aidha, alisema benki nyingi za biashara zinapenda kufanya biashara ya kununua hati fungani na kuziuza kwa faida kubwa na kuacha kutoa huduma za mikopo kwa wananchi wa kawaida.

Alitaka kuona wafanyabiashara ndogo (machinga) wananyanyuka kiuchumi kupitia mikopo yenye riba nafuu, na kuagiza kwamba riba isiwe kikwazo cha wananchi kukopa.

**AAGIZA UZALISHAJI WA MAKAA YA MAWE**

Akizungumza katika ufunguzi wa mtambo wa kuchenjua dhahabu uliogharimu Sh. bilioni 12.2, Rais Samia aliagiza mgodi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na Liganga uliodumu zaidi ya miaka 10 bila kuanza uzalishaji kuanza kazi.

Alisema mgodi huo umekuwa 'kizungukuti' na kwamba wakati umefika sasa uanze kufanya kazi na kama mwekezaji hataweza kukubaliana na sheria za serikali apewe mwekezaji mwingine.

Rais Samia alisema serikali imeshakutana na mwekezaji huyo na kufanya naye mazungumzo na kwamba ana imani mradi huo utaanza uzalishaji wa makaa ya mawe ili kupata nishati.

**WACHIMBAJI WADOGO**

Aidha, Rais Samia aliagiza wachimbaji wadogo kusaidiwa ili kufanya uchimbaji wa dhahabu na kuchangia pato la taifa, huku akitaka watengewe maeneo ya kuchimba.

Kuhusu uzalishaji wa madini ya Tanzanite, Rais Samia alitaka uwekwe mkazo wakipekee katika kuyatangaza na kuyauza nje ya nchi kwa kuwa yanapatikana Tanzania pekee.

Alisema licha ya kuongeza mkazo kwa madini ya dhahabu na almasi, lakini bidhaa hizo zipo katika nchini nyingine tofauti na Tanzanite ambayo duniani inapatikana Tanzania pekee.

Akizungumza katika uzinduzi wa jengo la BoT, Kaimu Waziri wa Fedha na Mipango ambaye ni Waziri wa Mdini, Dotto Biteko, alisema mapato ya serikali yamepanda kutoka Sh. bilioni 850 kwa mwezi mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa Sh. trilioni 1.4 kwa mwezi.

Aidha, alisema watu wazima wanaotumia miamala ya fedha mwaka 2017 walikuwa asilimia 65 kutoka asilimia 45 ya mwaka 2009.

Aidha, alisema teknolojia ya kisasa ya malipo imesaidia kukuza mapato ya serikali, huku akitaka BoT kuendelea kubuni njia za kukuza uchumi.

Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga, alisema jengo hilo la kisasa lina sehemu maalum kwa ajili ya kuchakata noti.

Alisema jengo hilo litahudumia mikoa saba ya Kanda ya Ziwa, na kwamba BoT itaendelea kutoa ushauri wa kukuza uchumi kupitia mipango na sera mbalimbali.

Rais Samia leo anaendelea na ziara yake jijini Mwanza kwa kuzindua ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Mwanza hadi Isaka mkoani Shinyanga, mradi wa maji wilayani Misungwi na kukagua ujenzi wa Daraja la JPM la Kigongo - Busisi.

# Ni wiki ya kujadili bajeti bungeni

**Na Salome Kitomari**

NI wiki ya mjadala wa kuchambua mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2021/22 yaliyowasilishwa bungeni wiki iliyopita na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.

Mjadala huo unatarajiwa kuanzia leo hadi Juni 22, mwaka huu na kuhitimishwa kwa kupiga kura ya wazi ya kupitisha bajeti na kufuatiwa na Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2021.

Dk. Nchemba aliwasilisha mapendekezo ya bajeti hiyo iliyoonyesha maeneo ya kupunguza, kuondoa kodi huku kukiwa na vyanzo vipya vya mapato.

Maeneo yanayotarajiwa kuwa na majadala kwa wawakilishi hao wa wananchi ni katika kodi ya laini za simu, miamala na kodi ya majengo ambayo itatozwa kupitia malipo ya Luku za umeme kila mtumiaji atakavyoweka.

Waziri Mwigulu alipendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Majengo, ili ukusanyaji ufanyike kwa kutumia mfumo wa ununuzi na utumiaji wa umeme kupitia mashine za Luku itakayokatwa kwenye ununuzi wa umeme.

Alisema kila mita ya umeme ina uhusiano na mmiliki wa jengo au mtumiaji wa mita, na kwa kuwa sheria ya kodi ya majengo inataka kodi hiyo ikusanywe kwa mmiliki au mtumiaji wa jengo.

"Napendekeza kodi ya majengo ya kiwango cha Sh. 1,000 kwa mwezi kwenye nyumba za kawaida zenye mita moja, Sh. 5,000 kwa mwezi kwa kila ghorofa au 'apartment' zenye mita moja. Serikali itaweka utaratibu kwenye nyumba za kawaida na za ghorofa zinazochangia mita moja na zinazotumia mita zaidi ya moja," alisema.

Mapendekezo mengine ni kutoza tozo ya Sh. 10 hadi Sh. 10,000 katika kila muamala wa kutuma au kutoa pesa, na kwamba kiasi kinatofautiana kulingana na thamani ya muamala wa fedha unaotumwa au kutolewa na lengo ni kukusanya Sh. milioni 1,254,406.14.

Aidha, mengine ni kutoza kiasi cha Sh. 10 hadi Sh. 200 kwa siku kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji. Ili kukusanya Sh. milioni 396,306.0.

Mjadala wa wabunge ndiyo utawezesha mabadiliko au kupita kama ilivyopendekezwa kwa bajeti hiyo ambayo imeangazia zaidi kuondoa na kupunguza kodi kwa bidhaa za ndani ili kustawisha viwanda vya ndani.

"Nasubiri kwa hamu namna ambavyo wawakilishi wetu bungeni watakavyojadili bajeti hasa katika kodi ya laini za simu na miamala, pia namna serikali italifafanua kwa kuwa halieleweki vizuri," alisema Caroline Joseph, mkazi wa Salasala, Dar es Salaam.


Katika mwaka mpya wa fedha serikali imepanga kukusanya Sh. trilioni 36.26

HABARI KITAIFA

# Wasomi wanavyomlilia Profesa Baregu

**Na Salome Kitomari**

WASOMI, wanasiasa na watu mbalimbali wamemlilia mwanazuoni na mwanasiasa, aliyekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Profesa Mwesiga Baregu (pichani), aliyefariki dunia jana.



Baadhi waliandika kwenye mitandao ya kijamii na walioongea na Nipashe, wamemwelezea kiongozi huyo alivyokuwa mwanazuoni mahiri na Afrika imepata pigo kubwa.

Baregu ambaye alikuwa Profesa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alikutwa na mauti akiendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alikokuwa amelazwa tangu Februari 16, mwaka huu, alikuwa chumba cha uangalizi maalum (ICU) kwa siku 15.

Profesa wa Sheria na Katiba wa UDSM, Issa Shivji, alisema Profesa Baregu atakumbukwa kama mwanazuoni wa muda mrefu ambaye aliandika machapisho ya masuala mengi hasa ya demokrasia, ambayo ataendelea kukumbukwa.

Alisema alimfahamu kama mwanazuoni wa muda mrefu akiwa UDSM ambaye alishiriki mambo mengi ikiwamo mijadala.

Naye Mwanazuoni na Waziri wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo, aliandika kwenye ukurasa wake wa twitter kuwa "Pumzika kwa amani msomi ambaye uliamini sana kwamba wasomi hawapaswi kujitenga na siasa. Ulitufundisha baadhi yetu ambao tulikubaliana nawe kuwa wasomi wanaweza kufanya siasa halisi bila kupoteza ukali wao wa kiakili."

Naye Mwanasiasa na Waziri mstaafu, Profesa Anna Tibaijuka, aliandika "Shemeji yangu Prof. Baregu ni urithi usiopingika kwa kuweza kusawazisha fikra za kuwa mwanasiasa na msomi bia kujali hatari zilizopo kwa kuwa sehemu ya chama huku ukiwa mkweli na mwadilifu, ulisimamia ulichokiamini. Rambirambi zangu kwa familia."

Naye mwandishi wa vitabu Mwalimu Richard Mabala, aliandika "Apumzike kwa amani Prof. Baregu, gwiji mbobevu aliyekuwa tayari kuishi kulingana na msimamo wake licha ya misukosuko aliyopewa."

Balozi Togolani Mavura aliandika "Ulale mahala pema Prof. Baregu nitaendelea kukumbuka kwa ile dhana uliyonifundisha pale UDSM kuhusu mlinganyo wa mshiriki, maslahi na mkakati katika kuchambua na kutafuta suluhu katika mgogoro wowote."

Tumaini Makene aliandika "Wakati fulani mwaka 2009/10 ulinipa fursa ya mahojiano maalum, ukanieleza mapambano ya maisha yako, chuoni, urafiki wako na Robert Mugabe (aliyekuwa Rais wa Zimbabwe), mahaba yako kwa Bob Marley. Utabaki mmoja wa wanazuoni mahiri tuliobarikiwa kuwa nao."

Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliandika "Prof. Mwesiga Baregu, Mwenyezi Mungu akuhifadhi mahala pema peponi Amina. Tanzania imepoteza mwanazuoni wa umma."

**CHADEMA WAMLILIA**

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, ilisema chama hicho kimepoteza mwanachama mwandamizi na aliyekuwa mjumbe wa Kamati Kuu.

"Tumepokea kwa majonzi na huzuni kubwa taarifa za kifo cha Prof. Baregu ambaye aliwahi kuwa mwanazuoni mahiri katika taifa letu na Afrika kwa ujumla ambaye amejipambanua katika kauli na matendo kupigania haki, utu, demokrasia na heshima ya mwafrika popote alipokuwa na alisimama mahiri katika hilo hadi umauti unamfika," alisema na kuongeza:

Kwa mujibu wa Mnyika, Prof. Baregu ni miongoni mwa wanazuoni waliosimama imara kupigania mfumo wa vyama vingi nchini, kuuasisi na kuuishi wakati wote bila kuyumba akiamini pia katika hitaji la nchi la kupata Katiba Mpya itakayotokana na maoni ya wananchi wenyewe na alisimamia msimamo akiwa Mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

"Tunatoa pole kwa familia na Watanzania kwa kumpoteza mzalendo wa kweli na mpigania demokrasia mahiri, tunatoa pole kwa wanazuoni wa tasnia na wanamajimui wa Afrika kwa kuondokewa na msomi mbobezi na mwana halisi wa Afrika," alisema Mnyika.

Kuhusu taratibu za mazishi, alisema CHADEMA itaendelea kutoa taarifa kwa kadri inavyoshauriana na familia.

Aliwahi kufanyakazi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), baadaye alihamia Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUT) na alikuwa Mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoongozwa na Jaji Joseph Warioba na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA.

## KUPOTEA KWA CHETI



**EDWARD S. MALINGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0061** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia MZINGA SEKONDARI mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/TAB/RB/289468/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOSHI**
**Kituo cha UCHIRA Mkoa KILIMANJARO**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 7/2021.**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU AIKASIA DAVID KILAWE WA KIRUA VUNJO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ABEL DAVID ELISONGUO**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama ya Mwanzo).**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 Mwezi 06 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.

He land Disputes courts (The District land and Housing Tribunal)RegulationsGN.No.174/2003

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**KIGOMA**
**MAOMBI NO 36 MWAKA 2021**

**ISSA POYONGO NYOKA**
**MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**KAPIPI ALLY,BIDYANGUZE GROUP TANZANIA LTD**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 21 mwezi wa 7 mwaka 2021 saa 2:30nasubuhi/mchana mbele ya muheshimiwa **F. CHINUKU** Mwenyekiti wa Baraza .Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wanguna Lakiri/muhuri wa Barazahili leo tarehe 9 Mwezi wa 6 Mwaka 2021

MWENYEKITI



# Majaliwa awaagiza ma-RC, DC, wakurugenzi kilimo cha alizeti

**Na Elisante John, SINGIDA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, maofisa kilimo na maofisa ushirika kushirikiana katika kusimamia kilimo cha alizeti.

Amewataka kuhakikisha nchi inaondokana na utegemezi wa kuagiza mafuta ya kula kutoka nje.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wadau wa zao hilo na kueleza kwamba hakuna sababu ya kuagiza mafuta ya kula nje kwa sababu nchi ina ardhi nzuri pamoja na nguvu kazi ya kutosha.

"Lengo la serikali ni kuongeza uzalishaji na tija kwa kuimarisha utafiti, huduma za ugani, upatikanaji wa mbegu bora na viuatilifu, kuongeza matumizi ya zana bora za kilimo, kuwajengea uwezo wazalishaji kuhusu kanuni za kilimo bora, kuanzisha mfumo imara wa ugharamiaji wa mazao ya mafuta kwa kushirikisha taasisi za fedha," alisema Majaliwa.

Majaliwa alisema ni matarajio ya serikali kuwa mikakati hiyo itawezesha kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 649,437 hadi tani 1,500,000 za alizeti zitakazochangia upatikanaji wa mafuta kwa takribani tani 300,000 ifikapo mwaka2025.

Alisema mahitaji ya mafuta ya kula nchini yanakadiriwa kuwa ni tani 650,000 na uzalishaji wa ndani ni wastani wa tani 290,000 sawa na asilimia 45 ya mahitaji kwa mwaka.

Aliongeza kwamba nchi hulazimika kuagiza wastani wa tani 360,000 hadi tani 400,000 kwa mwaka kufidia upungufu huo.

Majaliwa alisema uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje kwa mwaka hugharimu Sh. bilioni 474.

Waziri Mkuu alisema kutokana na umuhimu wa mafuta ya kula, serikali imeweka mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta yakiwamo ya chikichiki, alizeti, pamba, karanga na ufuta ili kujitosheleza na kuondokana na uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi.

Alisema awali serikali ilianza kutekeleza mikakati ya kuendeleza zao la michikichi kwa kuweka nguvu katika Mkoa wa Kigoma kwa kuanzisha Kituo maalum cha Utafiti wa Mchikichi cha Kihinga.

Pia alieleza kwamba serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeamua kulipatia uzito unaostahili zao la alizeti kwa kuwaunganisha wadau na kuanzisha kampeni ya kilimo bora cha alizeti pamoja na kuhamasisha viwanda vya kukamua mafuta kwa kuboresha teknolojia kwa viwanda vilivyopo na kuanzisha viwanda vipya kulingana na mahitaji.

Kadhalika, aliwahamasisha wananchi kulima zao la alizeti ili waweze kujiongezea kipato.

"Kama unataka utajiri wa haraka ndani ya miezi mitatu, minne lima alizeti kwa sababu kilimo chake si kigumu. Kwa hiyo ukitaka fedha ya haraka, nzuri na ya uhakika na yenye faida kubwa lima alizeti," alisema Majaliwa.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alisema serikali imeweka mkakati wa kuboresha huduma za ugani kwa kuongeza bajeti ili kuhakikisha wakulima wa zao hilo wanalima kilimo bora na kuongeza tija kwenye uzalishaji.



Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kushoto), akimpongeza Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba nje ya ukumbi wa Bunge baada ya kutoka kuwasilisha Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka 2021/2022 Bungeni jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto ajinyonga kwa kamba chumbani

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MTOTO Yassin Kalolo (14), mkazi wa Ipogolo, Manispaa ya Iringa mkoani Iringa, amekutwa amejinyonga kwa kutumia kamba chumbani.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kwamba Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa kifo chake kwani hakukuwa na ujumbe wowote ulioachwa na mtoto huyo.

Mashuhuda wa tukio hilo walilieleza Nipashe kuwa tukio hilo lilitokea Juni 12, majira ya saa 12 jioni wakati mama mzazi wa mtoto huyo akiwa jikoni.

Walieleza kuwa wakati mzazi wa mtoto anaendelea na shughuli za jikoni ghafla alisikia kishindo kikubwa cha mlango, alipoingia ndani ndipo alipomkuta mtoto huyo akiwa amejinyonga.

Shuhuda mwingine, Stella Fweni, alisema kifo cha mtoto huyo ni cha ajabu kwani haijapata kutokea mtoto mdogo kujinyonga katika mazingira hayo.

Baba mkubwa wa mtoto huyo, Ally Kalolo, alisema kuwa kabla ya kutokea kwa tukio hilo mtoto huyo ambaye alikuwa ni mwanafunzi wa darasa la nne alikuwa amemwomba Sh. 500 kwa ajili ya kwenda kulipia mtihani wa kila Jumamosi shuleni.

Alisema baada ya kumpatia kiasi hicho majira ya asubuhi hakuweza kuonana naye hadi walipopewa taarifa ya kifo chake.

Kalolo alisema hadi sasa hafahamu ni kitu gani kimesababisha mtoto huyo kufikia uamuzi wa kujinyonga, kwani tabia yake siku zote ilikuwa nzuri na hakuwa mtoto mwenye tabia mbaya.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Ipogolo, Furaha Mlagala, akithibitisha tukio hilo kwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa alisema tukio hilo ni la kwanza kutokea katika mtaa na wanaendelea kufanya uchunguzi kubaini chanzo.

# Serikali kuendelea kuiwezesha ATCL

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imejipanga kuhakikisha ya kwamba huduma za usafiri wa anga wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) zinaimarika na kuendelea kuwezeshwa ili itimize majukumu yake kikamilifu.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamriho, alisema hayo kupitia hotuba yake iliyosomwa na Naibu Waziri wake, Mhandisi Godfrey Kasekenya, mjini Morogoro wakati wa uzinduzi na ufunguzi wa kikao cha kwanza cha baraza jipya (baraza la pili) la wafanyakazi wa ATCL.

Dk. Chamriho alitaja majukumu hayo ni pamoja ununuzi wa ndege tatu (bombardier moja na Airbus mbili) ambao unatekelezwa kama ilivyopangwa.

Alisema, zabuni za ununuzi wa ndege tano zaidi ikiwamo moja ya mizigo zikitarajiwa kuhitimishwa kabla ya kumaliza kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021.

Alisema serikali itaendelea kujenga uwezo wa shirika hilo ili lichangie zaidi katika ukuaji wa uchumi wa Taifa na kufanikisha sera ya viwanda.

Waziri pia alisema, serikali itaendelea kushughulikia madeni ya ATCL yanayoendelea kuathiri ufanisi wake.

Waziri hiyo alisema, baada ya mafanikio makubwa waliyopata hasa katika miundombinu na mifumo mbalimbali ya uongozi, usimamizi na uendeshaji, pamoja na changamoto zake, upo umuhimu wa kulenga nguvu ili kujiimarisha sokoni.

## TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MARUDIO:

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA KUJENGA NYUMBA MBADALA KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMBUKUMBU NA: 0010006840

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya Mafuta na Gesi, inaalika makampuni yenye uzoefu na sifa kutuma nia ya kujenga nyumba mbadala kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati hizo kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Katika upande wa Tanzania bomba litapita katika mikoa nane (8), halmashauri za wilaya 27 na vijiji 231.

### MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

Ujenzi wa nyumba mbadala na majengo tegemezi (jiko na vyoo) kwa Waguswa wa Mradi (PAPs) wanaohamishwa na Mradi wa Bomba utafanyika katika mikoa nane tofauti; Kagera, Tabora, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Manyara na Dodoma.

Mradi utajenga nyumba mbadala katika ardhi iliyokubalika kwa waguswa stahiki wanaohamishwa makazi. Mradi utabainisha aina za muundo wa majengo mbadala yatakayojengwana maeneo kwa makubaliano na kila Mguswa wa Mradi. Mkadarasi atajenga nyumba 336, Vyoo vilivyoboreshwa vyenye mfumo wa kuzungusha hewa 388 na majiko ya nje 345 kutokana na michoro iliyosanifiwa kwa kina na Kampuni ambayo yote imeandaliwa kwa viwango vya usawa vya ujenzi wa nyumba.

Muundo wa chini na juu (msingi uliofungwa nondo na kumwagiwa zege, kuta za ndani/nje) kwa kila nyumba pamoja na nyumba tegemezi zitajengwa kwa kutumia vifaa vya vipimo vitakavyotolewa na Kampuni na vinavyoweza kutumika zaidi ya mara moja na kwa kutumia mseto wa zege uliosanifiwa kwa kazi husika.

Wakandarasi wote watategemewa kufanya kazi kwa kutumia mfumo huu wa vifaa vya vipimo vitakavyotolewa. Ukamilishaji wa kazi yote inayobakia (vibarua na rasilimali) kama vile kupaua, kukamilisha ujenzi, umeme na miundo mbinu ya maji safi na maji taka, kazi za ujenzi na uboreshaji wa muonekano wa ardhi zitakuwa ni jukumu la Mkandarasi.

Wazabuni watakao kidhi vigezo vya awali watapokea taarifa za muundo wa vifaa vyenye vipimo vitakavyoonyesha wazi na kuwa na taarifa za kina juu ya utengenezaji wa bidhaa husika.

Nyumba mbadala kwa ujumla zitakuwa zina kati ya vyumba viwili mpaka vitano, vyenye ukubwa wa eneo la sakafu wa mita za mraba 25 mpaka 75. Kila nyumba itakuwa na miundombinu tegemezi miwili, yaani jiko na choo cha shimo kilichoboreshwa chenye mfumo wa kuzungusha hewa. Nyumba mbadala zitakuwa za kiwango bora cha ujenzi. Kwa muundo wa chini na juu wa nyumba, nyumba zote zitajengwa kwa kutumia malighafi zinazopatikana katika maeneo husika, zote zitakidhi viwango vya ujenzi vya ubora vya Tanzania .

### VIGEZO MUHIMU:

Kutokana na ukubwa wa kazi na ili kuyasaidia makampuni yanayoonyesha nia, Mradi una haki ya kutoa kazi moja moja au pia kazi zaidi ya moja kwa mkandarasi atakayeonyesha nia na mwenye kukidhi vigezo. Kampuni zenye nia zinaweza kuingia mikataba na kampuni nyingine ili kuwezesha uwezo wao wa kutoa huduma, lakini wote kwa Pamoja na kila mbia katika mkataba ni LAZIMA akidhi matakwa tajwa yaliyoainishwa hapo chini.

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Kampuni ya Kitanzania ya Ukandarasi (Ujenzi) iliyosajiliwa kwa kiwango cha chini cha daraja la pili (wasilisha nakala),
- Mifano ya uzoefu wa kujenga majengo katika mkoa wa Kagera, Tabora, Geita, Shinyanga, Singida, Manyara na Dodoma Tanzania. (Wasilisha orodha ya miradi iliyofanyika katika mkoa wowote tajwa au mikoa yote),
- Thibitisha uwezo wa kifedha wa kutekeleza kazi tajwa,
- Thibitisha/wasilisha sera za Afya, Usalama na Mazingira (HSE/OSHA), na Usimamizi wa Viwango vya Ubora na maswala ya Jamii,
- Wasilisha/Thibitisha uzoefu wa kusimamia miradi, utaratibu wa ugavi na usafirishaji vitu Pamoja na manunuzi,
- Dhamira ya kuongeza thamani katika uwezo wa ndani/taifa (wasilisha taarifa za kina za mafunzo),
- **Uthibitisho wa usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) ya EWURA wakati wa kuwasilisha taarifa ya nia unahitajika.**

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: tolal.mufti@external.total.com (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **15 Julai 2021.**

Taarifa ya kina itawasilishwa na Kampuni ili kutoa taarifa zaidi kuhusu huduma, ratiba ya utekelezaji pamoja na kutoa kipindi cha maswali na majibu kutoka kwa wazabuni wenye nia - undani wa taarifa utawasilishwa katika hatua ifuatayo.

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya Makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kanuni uchaguzi Mkuu TFF ziheshimiwe, haki itendeke

**HATIMAYE** dirisha la kuchukua na kurejesha fomu kuwania uongozi wa juu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), limefungwa rasmi Jumamosi Juni 12, mwaka huu, huku kipengele cha 'Endorsement' (dhamana/kudhaminiwa) kikionekana kuwa kikwazo kwa wagombea wengi.

Baadhi ya wagombea wameshindwa kukidhi kipengele hicho cha kupata ridhaa kutoka kwa vyama, mikoa na klabu zenye dhamana ya kupiga kura katika uchaguzi huo utakaofanyika jijini Tanga Agosti 7, mwaka huu.

Katika nafasi ya kiti cha urais wa shirikisho hilo, kati ya wagombe 10 waliochukua fomu ni sita tu ambao wamezirejesha, lakini baadhi yao wakilalamika kutokana na kushindwa kufikisha idadi ya wadhamini angalau watano kama ambavyo kanuni inasema.

Wagombea waliorejesha fomu katika nafasi ya urais ni Ally Mayay Tembele, Ally Saleh, Evans Mgeusa, Hawa Mniga, Oscar Oscar na Rais anayetetea kiti chake, Wallace Karia, huku Mwenyekiti wa zamani wa Yanga na Mbunge wa Kinondoni (CCM), Abbas Tarimba, Mbunge wa Jimbo la Mwera mjini Zanzibar, Zahor Mohammed Haji, Deogratius Mutungi na Rahim Kangezi wakishindwa kurejesha fomu hizo.

Kwa upande wa nafasi ya Wajumbe wa Kamati ya Utendaji kwa kanda zote sita waliorejesha fomu ni Athuman Kingome Kambi, Elisony Mweladzi, Jimmy Shomari Msindo, Lameck Nyambaya, Liston Katabazi, Saady Mohamed Khimji, Hosseah Lugano, Khalid Abdallah Mohamed, Zakayo Mjema na Thabithy Kandoro.

Wengine waliorejesha ni pamoja na Abousufian Sillia, James Mhagama, Joseph Ngunangwa, Ulisaja Elias, Denis Manumbu, Mohamed Mashango, Hamisi Juma Kitilia, Mohamed Aden, Osuri Kosuri, Mrisho Ramadhani Kibwigiri, Salum Umande Chama, Vedatus Lufano, Salum Alli Kulunge, Blassy Kiondo, Issa Mrisho Bukuku na Kenneth Pesambili.

Hiyo ni hatua ya kwanza, hivyo kinachofuata sasa ni kuangalia utekelezwaji wa kanuni ya udhamini pamoja na kukamilishwa kwa vigezo vingine ikiwa ni pamoja na uzoefu katika soka, lakini ujazwaji sahihi wa fomu hizo na sifa nyingine kwa mgombea ikiwamo elimu.

Tunatambua yapo malalamiko mengi ambayo tayari yamewafanya baadhi kukosa sifa ya kurejesha fomu ikiwamo hilo la wadhamini, lakini wengi wataendelea kulalamika baada ya kuenguliwa katika hatua inayofuata kutokana na kushindwa kukidhi vigezo.

Nipashe tunachotaka kukiona ni haki ikitendeka lakini si kutendeka tu bali ionekane kweli ikitendeka kwa kufuata kanuni/sheria za uchaguzi huo kama zilivyoainishwa bila kumwonea yeyote.

Hatutaki kuona kanuni/sheria za uchaguzi zikipindishwa/kukanyagwa kwa sababu ya kumbeba yeyote yule, na watakaokosa sifa ama kushindwa hawana budi kukubaliana na matokeo na kurejea kujipanga upya kwa baadaye kupendekeza mabadiliko ya katiba ambayo wanaamini yatakuwa rafiki zaidi kwa kila mmoja.

Kinachotushangaza ni ukimya wa wadau wa soka na kutokana na umuhimu wa kufuatilia ama kutoa mapendekezo yao wakati wa uundwaji wa kanuni/sheria za uchaguzi na badala yake kuibua hoja kama hizo wakati huu wa uchaguzi ambao haiwezekani kufanya marekebisho kwa sasa.

Tunatarajia wadau na wanafamilia wote wa soka nchini watakubaliana na matokeo ama kitakachoamuliwa na Kamati ya Uchaguzi chini ya Mwenyekiti wake, Kiomoni Kibamba, ambaye tunaamini atasimamia haki itendeke.

Kama wapo ambao hawataridhika na mchakato mzima wa uchaguzi huo, basi wafuate taratibu ngazi kwa ngazi hadi ngazi ya mwisho ambayo ni Mahakama ya Usuluhishi ya Mambo ya Michezo (CAS) na si kuanza kukimbilia mahakama za kiserikali kwani kwa kufanya hivyo si tu watakutana na kifungo kikali, bali pia watalisababishia soka letu kuingia matatizoni kutoka Fifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kongole serikali kuondoa kodi nyasi bandia

**WAKATI** akiwasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22 Bungeni jijini Dodoma Juni 10, mwaka huu kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa, pamoja na mambo mengine serikali ilipendekeza kusamehe ongezeko la thamani kwenye nyasi bandia kwa viwanja vya mpira wa miguu kwenye majiji kwa ajili ya kuendeleza michezo na kukuza vipaji nchini.

Akisoma bajeti hiyo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema kwa mwaka huu wa fedha, anapendekeza kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye nyasi bandia kwa ajili ya viwanja vya mpira wa miguu vya majiji, huku kukiwa na lengo la kufanya hivyo kwenye manispaa, viwanja hadi kwenye timu wakati wa bajeti zijazo.

"Mheshimiwa Spika, viwanja vyetu vingi ni vibovu sana, labda ukiacha kile cha Majaliwa Lindi.

Vingi ni vibovu. Na ubovu wa viwanja hivyo unasababisha timu bora kama Yanga inashindwa kupata matokeo mazuri inapokwenda mikoani," alisema waziri huyo na kusababisha vicheko na makofi kutoka kwa baadhi ya wabunge.

Hapa waziri aliingiza kidogo utani wa jadi wa Simba na Yanga kama kawaida, kwani inajulikana Dk. Nchemba ni shabiki mkubwa wa Yanga.

"Napendekeza kusamehe ongezeko la thamani kwenye nyasi bandia zinazotambulika kwa HS Code 5703.30.00 na 5703.20.00 kwa ajili ya viwanja vya mpira vilivyoko kwa kuanzia kwenye majiji.

Msamaha huo utahusisha ridhaa kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF). Ni jambo ambalo Waziri wa Sekta hiyo amelipigania sana. Lengo la hatua hii ni kuendeleza michezo na kukuza vipaji hapa nchini. Tukifanikiwa kwenye majiji, bajeti zinazofuata tutakwenda manispaa, kwenye viwanja hadi kwenye timu," alisema.

Binafsi, napenda kuipongeza serikali kwa kuliona hilo kwani hicho ndicho kilio kikubwa cha muda mrefu cha mashabiki na wapenzi wa michezo nchini.

Ikumbukwe hata Simba nyasi zao bandia zilizojenga Uwanja wa Mo Simba Arena, zilikaa bandarini kwa siku nyingi, pamoja na sababu zingine, lakini kodi nayo ilichangia sana.

Wengi hawakutarajia hilo, kwani kwenye Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, baadhi ya wabunge badala ya kuzungumzia kero za jumla, au matatizo yanayosababisha soka la Tanzania lisipige hatua, wao wakawa wanalilaumu Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuwa ndiyo linasababisha hivyo.

Wengine wakaleta itikadi zao za Usimba na Uyanga, badala ya kuieleza serikali iangalie pale inapoweza kulisaidia soka la Tanzania kupiga hatua.

Ni Wabunge wachache sana ambao moja kwa moja waliishauri serikali jinsi ya kufanya ili michezo kwa ujumla Tanzania isonge mbele.

Hawa kwa kiasi kikubwa ndiyo walioiamsha serikali kuangalia jinsi gani ya kufuta kodi ya nyasi bandia. Nilizungumza kwenye safu hii wiki iliyopita kuwa soka la Tanzania lina matatizo mengi, na kulaumu TFF kuwa ndiyo chanzo ni kuionea tu.

TFF haimiliki viwanja. Viwanja vingi vimekuwa vikimilikiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na watu binafsi. Viwanja vingi ambavyo vinachezewa Ligi Kuu Tanzania Bara vimekuwa na ubora usioridhidhisha sehemu za kuchezea.

Kwa maana hiyo, ujio wa nyasi bandia ambazo hazitokuwa na kodi, zinaanza kwanza kwenda kutandikwa kwenye viwanja vya majiji ili kufanya kwanza wachezaji wetu waonyeshe vipaji halisi na timu zishinde kutokana na uwezo uwanjani pamoja na mfumo wa mwalimu na si faida ya uwanja mbovu.

Dk. Mwigulu alitolea mfano Yanga kuwa haifanyi vema mikoani kwa sababu ya viwanja vibovu, lakini si timu hiyo tu. Timu zote kubwa kama Simba, Yanga, Azam na zile zenye falsafa ya kuweka mpira chini, zimekuwa zikiathiriwa sana na viwanja vya mikoani ambavyo vingi vimekuwa na nyasi hafifu, zenye mwonekano mbaya, na udongo mgumu unaofanya mpira kudundadunda, badala ya kutambaa.

Hali hii inasababisha wachezaji hasa wa timu za mikoani, kuwa na kazi moja tu ya kupiga mipira juu na kukimbizana badala ya kucheza kwa mfumo sahihi uliotengenezwa na makocha wao.

Matokeo yake nchi inakosa wachezaji 'mafundi' kama kina Clatous Chama, Haruna Niyonzima, Saido Ntibazonkiza, Luis Miquissone na Rally Bwalya.

Ninaamini nyasi bandia zitakapotandikwa kwenye viwanja vyote vibovu, baada ya miaka kadhaa tutaanza kuona matunda ya haya ambayo serikali imeyafanya kwenye bajeti ya mwaka huu.

HABARI KITAIFA

# Naibu Meya asitisha utoaji leseni baa makazi ya watu

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Meya wa Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Kheri Missinga, amewaagiza maofisa wanaohusika na utoaji leseni za biashara kusitisha leseni ya baa moja iliyopo karibu na shule na makazi ya watu kwa kutofuata sheria.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati akiongea na wajumbe wa kamati ya vileo katika ofisi za Manispaa ya Kinondoni. Pia kikao hicho kiliwajumuisha baadhi ya majirani wanaoishi jirani na baa hiyo iliyopo Mbezi Beach, Kata ya Kawe, wilayani Kinondoni.

Alisema kamati ilifikia uamuzi wa kutoipa leseni baa hiyo, baada ya wananchi wa eneo hilo kufika katika Ofisi za Manispaa ya Kinondoni na kutoa malalamiko ya kumtaka mmiliki wa baa (night club), kusitisha biashara hiyo kwa madai ya kusababisha kelele za muziki kwa wanafunzi na majirani.

Pia alisema ofisi yake imethibitisha eneo hilo siyo sahihi kwa uendeshwaji wa biashara ya baa kutokana na mazingira na kuwataka maofisa wanaotoa leseni za biashara kukagua eneo na kujiridhisha kama inakidhi vigezo kabla ya kutoa leseni.

"Katika eneo lile kuna mambo mawili, la kwanza ni sauti inawasumbua majirani, pili ni mazingira, wale watu wakiwa tayari wameshapata vitu vyao kuna mlango ule wa watoto wa shule kuna vitu vinadondoka dondoka ambavyo sio vizuri kwa maadili ya watoto wetu wakiviona," alisema.

"Sisi tulikuwa hatujui kuwa anaendesha baa pale baada ya kwenda kukagua ndiyo tukagundua na tulimpiga faini ya Shilingi milioni moja na maamuzi yetu ambayo tumeyafikia, kwanza avunje jukwaa la bendi aliloliweka nje, asimamishe biashara hiyo na asipewe leseni," alisema.

Kwa upande wake Ofisa Mipango Miji wa Manispaa ya Kinondoni, Emmanuel Masanyiwa, alisema kwa maana ya tafsiri ya sheria ni kuwa biashara katika eneo hilo hairuhusiwi kwa sababu kiwanja hicho hakikufanyiwa mabadiliko ya matumizi.

"Mabadiliko ya matumizi ya kiwanja hayakuidhinishwa na Mkurugenzi wa Mipango Miji wa Wizara, bado msimamo wetu unabaki pale pale pamoja na masharti mengine lazima warudi katika mabadiliko ya sheria na bado sheria inamzuia mmiliki wa eneo hilo kubadilisha hadi hapo eneo litakapoidhinishwa na mkurugenzi," alisema.

Mmoja wa wakazi waliofika kwenye kikao hicho kupata ufafanuzi wa sakata hilo, ambaye hakupenda jina lake liandikwe gazetini, alisema baa hiyo inasababisha usumbufu kwa watoto na wanafunzi wanaosoma Shule ya Msingi Mbezi Beach, inayopakana na eneo hilo.

"Uwepo wa baa katika eneo hilo inaweza kusababisha watoto kufanya vitu kinyume na maadili kwa kuwa kila kinachofanyika katika baa hiyo ni rahisi kukiona," alisema.

# Shirika laitaka sekta binafsi uchumi wa bluu

**Na Elizabeth Zaya**

JUKWAA la Hiari la Umoja wa Mataifa la kushajiishia maendeleo endelevu(UN Global Compact), limesema kuna haja ya kushirikisha sekta binafsi katika kufikia uchumi wa bluu kwa kuwekeza zaidi katika matumizi sahihi ya rasilimali zilizopo katika bahari, mito na maziwa.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa jukwaa hilo, Saimon Shayo, katika mkutano wa mwaka wa jukwaa hilo wa kujadili namna ya kutumia rasilimali za viumbe vilivyopo kwenye maji kuimarisha uchumi wa bluu.

"Nchi nyingi zimeamua kujielekeza kutengeneza tija kwenye matumizi ya uchumi wa bluu na hususan kutumia rasilimali zinazopatikana kwenye maziwa, bahari, mito na maeneo mengine," alisema Shayo.

"Matumizi ya mazao ya uchumi wa bluu hayaepukiki kwa sababu moja ya namna ya kufanikiwa kwenye ujenzi wa nchi kupitia uchumi wa viwanda ni lazima kutumia uhifadhi wa vyanzo vya uchumi wa bluu, uhifadhi wa hali ya hewa, maendeleo ya teknolojia na namna inavyoweza kutumika katika matumizi ya kiasi."

Alisema kama nchi, kuna haja kubwa ya kuweka mazingira bora ya kufikia katika uchumi huo wa bluu.

"Zanzibar wamepiga hatua kutokana na namna walivyojiwekea mipango mizuri ya kuendea uchumi wa bluu na wanastahili kupongezwa na kama nchi tunahitaji kweli kuingia katika uchumi huu, lakini tunapaswa kuhakikisha kwamba tunaweka mipango imara kwa namna ambayo hatutavuna mazao hayo bila kuyaendeleza," alisema Shayo.

"Kama ni samaki, lazima tuhakikishe kwamba kuna ufugaji mpya, lakini kutokuvuna samaki wachanga na kuhifadhi maeneo ambayo samaki wanazaliana na tumeona kwamba ni fursa kubwa ambayo itasaidia Tanzania kufikia uchumi wa viwanda kama ilivyotarajiwa."

Katibu wa Chama cha Mwamvuli wa Wafugaji Viumbemaji Tanzania, Geofrey Rucho, alisema upungufu wa samaki unaojitokeza kwa sasa ni kutokana na uharibifu unaojitokeza kwenye maji.

Rucho alisema kuna haja ya wafugaji kufundishwa mbinu bora ya ufugaji wa samaki kibiashara ambayo itakuwa rafiki kwa mazingira.

# Serikali yaonya madereva bodaboda

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewaonya madereva wa bodaboda wanaoshiriki matendo ya uhalifu ikiwamo usafirishaji wa wahamiaji haramu, dawa za kulevya, mauaji na uporaji wa vitu kuwa atayekamatwa atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, wakati wa kikao maalumu kilichowashirikisha madereva wa bodaboda, daladala na bajaji kujadili mambo mbalimbali ikiwamo ushiriki wa bodaboda kwenye matukio ya uhalifu na kuzidisha abiria katika vyombo hivyo.

Chilo aliwaambia madereva hao kuwa taifa linawategemea kama nguvu kazi.

"Nawaasa bodaboda kuachana na matendo ya kihalifu, serikali tunawategemea sana vijana kama nguvu kazi, lakini kuna baadhi ya vijana siyo wote wanatumika katika matukio ya uhalifu ikiwamo ujambazi, dawa za kulevya na wengine wakitumika huko mipakani kusafirisha wahamiaji haramu sasa tusizitumie bodaboda zikaleta sura mbaya kama chombo cha kutumika kufanya uhalifu wakati lengo lake ni kutumika kujikwamua kiuchumi," alisema.

Akizungumza katika mkutano huo, Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, aliwaomba bodaboda kutii sheria za usalama barabarani huku wakisubiri mapendekezo ya Bunge kuhusu kila kosa kutozwa Sh. 10,000 kupitishwa.

"Serikali imesikia kilio chenu cha muda mrefu cha kushushiwa gharama ya faini kutokana na makosa ya barabarani, tunamshukuru Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kusikia kilio chenu nawaomba sasa mfuate sheria za usalama barabarani mkishirikiana na Jeshi la Polisi," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Justine Maseji, aliwaonya watu wanaoshiriki matendo ya kuteka na kuwaua madereva bodaboda huku akielezea kuwa yeyote anayejaribu kucheza na maisha ya Watanzania atashughulikiwa.

"Mpaka mwezi wa tatu tumekamata pikipiki 60, nitoe onyo kali kwa watu wanaopora mali za wananchi waache kufanya mambo ya ovyo ovyo tutachukua hatua kali, mtu anayetafuta dozi sisi tutapeleka dozi kali zaidi na wao wahalifu wanafahamu maana sio kila kitu tunaweka wazi wanazijua 'sindano' tunazopeleka," alisema.




# Serikali yatoa miezi 3 uendeshaji nyama, maziwa

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (pichani), ametoa miezi mitatu kwa Msajili wa Bodi ya Maziwa nchini na Bodi ya Nyama, kuweka mikakati imara ya uendeshaji wa biashara katika bodi hizo.

Alitoa agizo hilo jijini Dar es Salaam alipokutana na Bodi ya Maziwa na Nyama kwa ajili ya kutoa maelekezo mbalimbali.

Ulega alisema mpaka sasa serikali inatumia pesa nyingi kila mwaka kuagiza maziwa nje ya nchi na kwamba endapo kungekuwa kumewekwa mazingira mazuri ya uzalishaji wa maziwa hayo nchini, badala ya fedha hiyo kutumika kuagiza bidhaa hiyo nje ingetumika kuboresha uzalishaji wa maziwa ya ndani.

"Maziwa mengi yanapotea huko kwa wafugaji, lakini moja ya sababu kubwa ya maziwa hayo kupotea ni kutokana na kutokuwapo kwa mipango mizuri ya namna ya kuyakusanya au kuyapata, kwa sababu vibebeo vyenyewe vya maziwa hayo ni gharama kubwa kwa hiyo wengi wao wanashindwa kumudu kuvinunua," alisema Ulega.

"Sasa nakuagizeni, changamkeni. Tunataka vibebeo vya maziwa vienee huko kwa wazalishaji na mshirikiane na watu wa sekta binafsi, wenye viwanda vidogo na vikubwa kusambaza hizo, sambazeni vifaa vya kubebea maziwa kwa vikundi vya kinamama na vijana na mpite kwenye hizi halmashauri zenye mifugo," alisema Ulega.

"Tunataka hivi vikundi vya wafugaji vya kinamama na vijana watumie pesa zile za halmashauri za asilimia 10 wanazopewa wakusanye maziwa yaliyopo kule vijijini ili yachakatwe, kwa hiyo kitengo cha masoko mnatakiwa kuamka na kuleta matokeo makubwa."



Alisema serikali inatumia Sh. bilioni 14 kila mwaka kuagiza maziwa nje, na endapo kutakuwa na mipango mizuri, badala ya kiasi hicho cha fedha kutumika kuagiza bidha hiyo nje ya nchi, itatumika kwa ajili ya kuboresha mazingira ya ndani ya upatikanaji wa maziwa kwa wingi.

Msajili wa Bodi ya Maziwa, Dk. George Msalya, alisema uzalishaji wa maziwa nchini umeongezeka kutoka lita bilioni 3.1 mwaka 2019/2020 hadi lita bilioni 3.4 mwaka 2020/2021.

Pia alisema usindikaji wa maziwa hayo umeongezeka kutoka lita 203,600 kwa siku mwaka 2019/2020 hadi kufikia lita 208,000 kila siku mwaka 2020/2021.

# Magonjwa yasiyoambukiza yatishia nguvu kazi

**Na Christina Mwakangale**

ONGEZEKO la Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza (NCDs) nchini, ikiwamo ugonjwa wa moyo, kisukari na presha, yanatajwa kuhatarisha kupungua kwa nguvu kazi ambayo ni tegemeo katika uzalishaji na kukuza uchumi.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, anasema asilimia 10 ya ongezeko la kundi la walio na magonjwa yasiyoambukiza linapunguza asilimia 0.5 ya pato la taifa na kudumaza uchumi.

Dk. Gwajima aliyasema hayo juzi wakati akitoa hotuba yake kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye tukio la uzinduzi wa mitambo mipya ya tiba ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), jijini Dar es Salaam.

Aalisema ongezeko la wagonjwa wanaougua magonjwa ya moyo yanaongezeka kwa asilimia 26 nchini kwa mwaka na yasipodhibitiwa huathiri watu katika mifumo ya uzazi na uzalishaji mali.

"Takwimu za WHO mwaka 2005 zinaonyesha asilimia 30 ya vifo vinavyotokea kutokana na magonjwa haya vinatokea kwa watu walio na umri chini ya miaka 60.

"Hawa ndio nguvu kazi ya taifa letu. Kwa msingi huo magonjwa haya yasipodhibitiwa yatapunguza nguvu kazi na ufanisi, yataongeza mzigo kwa taifa, kuchochea umaskini katika ngazi ya familia," alisema Dk. Gwajima.

Alisema serikali imetenga kila Jumamosi ya wiki ya pili ya mwisho wa mwezi kuwa ya kufanya mazoezi, kwa sekta zote pamoja na kuwekwa mkakati wa kuhamasisha michezo kuepukana na NCDs.

Kadhalika, Dk. Gwajima alisema gharama ambazo serikali ilizitumia katika matibabu ya nje kwa magonjwa mbalimbali zilizofikia takribani Sh. bilioni 215, zimeokolewa baada ya kufunguliwa JKCI pamoja na kuboreshwa huduma za kibingwa hospitali nyingine nchini.

Alisema duniani takwimu za WHO zinasema vifo vinavyotokana na NCDs ni milioni 40 sawa na asilimia 71 ya vifo vyote, na robo tatu ya vifo vingeambuliwa mapema vingezuilika ama kutibika.

"Tanzania na nchi zinazoendelea inaonekana kuathirika na NCDs, yamesababisha vifo kwa asilimia 33 ya vifo vyote nchi mwaka 2017. Kwa vifo vyote magonjwa ya moyo na presha ilikuwa asilimia 13, kisukari asilimia mbili, saratani asilimia saba na ajali ni 11 asilimia," alisema Dk. Gwajima.

Tpb Bank
Grow with us

**TPB BANK PLC**

**TAARIFA KWA UMMA**

Ndugu wateja wetu na wadau wetu wote tunapenda kuwataarifu kuwa matawi ya iliyokuwa Benki ya TIB Corporate lililopo Mtaa wa Jacaranda mkoani Mbeya na Mlimani City mkoani Dar es Salaam yatafungwa tarehe 30 Juni 2021.

Wateja wetu waliokuwa wanatumia matawi haya kupata huduma mbalimbali za kibenki wataendelea kupata huduma hizo kupitia matawi ya Benki ya TPB yaliyoenea kote nchini.

**Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza**

# Hatimiliki ardhi kielektroniki Dodoma Julai

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

OFISI ya Ardhi Mkoa wa Dodoma itaanza kutoa hatimiliki za ardhi za kielektroniki kwa wamiliki wa ardhi kuanzia Julai mosi, 2021.

Hayo yamebainishwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma, Thadei Kabonga, wakati wa utoaji hati za ardhi 223 kwa wananchi waliorasimishiwa maeneo yao kwenye mitaa ya Miganga na Chinyika katika Kata ya Mkonze mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki.

Kwa mujibu wa Kabonga, kwa sasa ramani zote za mkoa wa Dodoma zipo kwenye mfumo wa kidijitali, hivyo ofisi yake itaanza kutoa hati za ardhi za kielektroniki kwa kuwa hati hizo ziko katika nakala laini.

Kwa sasa Wizara ya Ardhi imewekeza, imeboresha na kuongeza matumizi ya mifumo ya kidigitali ambapo tayari hati za kielektroniki nchini zimekuwa zikitolewa kwenye manispaa nne za mkoa wa Dar es Salaam ambazo ni Ilala, Temeke, Kinondoni na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo na hati hiyo ni ya kurasa moja.

"Ramani zote za Dodoma kwa sasa zipo kidigitali na Julai mosi mwaka huu tunaanza kutoa hati za kielektroniki maana hati zote ziko katika nakala laini," alisema Kabonga.

Aliwataka wakazi wa Dodoma wanaomiliki ardhi kuhakikisha wanapimiwa maeneo yao na kupata hati kwa kuwa gharama za upatikanaji hati sasa imepungua ukilinganisha na miaka ya nyuma na kusisitiza kuwa lengo la ofisi yake ni wananchi katika Jiji la Dodoma kupata hati zao.

Katika kuhakikisha ardhi ya Jiji la Dodoma inapangwa, inapimwa na kumilikishwa, Kamishna Kabonga alisema, ofisi yake ilipeleka timu ya wataalamu katika mitaa mbalimbali ikiwamo ya Miganga na Chinyika kwa lengo la kupima maeneo hayo lakini mwitikio wa wananchi umekuwa mdogo.

# Wadau alizeti waja na dawa kupunguza uagizaji mafuta

**Na Felix Andrew,**
MOROGORO

WADAU alizeti wamependekeza hatua kadhaa zinazopaswa kuchukuliwa na serikali kwa kushirikiana na washirika wengine, kwa lengo la kuongeza uzalishaji ili kupunguza uingizaji mafuta ya kupikia kutoka nje ya nchi.

Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha kwa mikataba ya kilimo, kupunguza kodi kwa wasindikaji wa mafuta, kuwasaidia wakulima na wasindikaji, kupunguza ushuru wa mbegu kutoka nje na kutumia mbegu zilizoidhinishwa.

Wakizungumza kwenye mkutano wa wadau wa zao la alizeti uliofanyika mkoani Morogoro, walisema juhudi zaidi zinahitajika kuchukuliwa na serikali hasa katika matumizi ya mashamba pori na kubadilisha sheria kadhaa ambapo pia wakulima wanatakiwa kuongeza uzalishaji na wadau wengine kama wazalishaji mbegu, wauzaji wa pembejeo na wasindikaji mafuta ya kupikia kufanya majukumu yao ipasavyo.

Mkutano huo uliitishwa na Baraza la Kilimo la Taifa (ACT) na kuwezeshwa na shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha kusaidia uendelezaji wa masoko ya kilimo (AMDT) na wadau wengine.

Pia wanachama wa kikundi cha uchambuzi wa sera kutoka Sagcot, ANSAF Dalbery na Aspires Tanzania) walikuwa ni sehemu ya mkutano.

Kwa mujibu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, mahitaji ya mafuta ya kupikia nchini yanakadiriwa kuwa ni mita za ujazo tani 570, 000 kwa mwaka ambapo ni tani za ujazo 205, 000 ndizo zinazalishwa kutoka ndani kwa sasa. Mbali ya kuwapo kwa fursa nyingi kwa uzalishaji wa alizeti, bado Tanzania inaagiza mafuta ya kupikia kutoka nje yapatayo mita za ujazo 365,000 kwa mwaka.

Mkulima Amina Dafi kutoka mkoani Singida, alisema Tanzania ina eneo kubwa la ardhi ambalo halitumiki na kuiomba serikali kuwapatia wakulima ili walime zao la alizeti. Alisema serikali inatakiwa kuhakikisha mashamba pori yaliyotekelezwa yanatumika kipaumbele hususani wanawake kwa ajili ya kilimo cha alizeti.

Mdau mwingine, Ringo Iringo, alisema

kwa sasa Tanzania ina upungufu mkubwa wa mbegu za alizeti, jambo linaloathiri uzalishaji wa mafuta ya kupikia. Akitolea mfano alisema uzalishaji wa mbegu kwa sasa ni tani za ujazo 500 kwa mwaka wakati mahitaji ni zaidi ya tani za ujazo 5,000 jambo linalosababisha baadhi ya wakulima kutumia mbegu za zamani (recycled).

Iringo ambaye ni Mwenyekiti cha Chama cha Wasindikaji wa Alizeti (TASUPA), alisema kuwa serikali inatakiwa kuhakikisha kuwapo kwa maofisa ugani kwa kila eneo ili kuwasaidia wakulima kutumia kanuni bora za kilimo.

Mkurugenzi wa uzalishaji kutoka Wakala wa Mbegu (ASA), Dk. Jackson Ringo, alisema serikali imeanza kuchukua hatua ili kuongeza uzalishaji na ubora wa mbegu, na kwamba kilimo cha umwagiliaji kitaanzishwa kwa baadhi ya mashamba ya mbegu na lengo ni kufikia uzalishaji wa tani 5,000 ifikapo mwaka 2023 kutoka tani chini ya 1,000 kwa sasa.

Tertula Swai, Mtaalamu wa Mazingira ya Biashara kutoka AMDT, alisema mkutano huo ulidhamiria kuja na suluhisho la kivitendo ambalo litaisaidia serikali kuja na mikakati ya muda mfupi na mrefu katika kusimamia hali ya mafuta ya kupikia nchini.

Akifungua mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa ACT, Timothy Mbaga, alisema juhudi zaidi zinahitaji kuimarisha tasnia ya alizeti.

Alisema kwa sasa uzalishaji wa mafuta ya kupikia nchini ni asilimia 40 na kuilazimu serikali kuagiza asilimia 60 kutoka nje kwa hiyo kuna umuhimu wa kubadili hali hiyo.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, akizungumza katika mkutano maalumu na waendesha mabasi, daladala, bajaji na bodaboda uliofanyika jijini Arusha jana, huku changamoto mbalimbali zilijadiliwa na kupatiwa ufumbuzi. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# Wenye ulemavu wataka kanuni za kutibiwa bure

**Na Lilian Lugakingira,** MULEBA

WATU wenye ulemavu wilayani Muleba mkoani Kagera, wameiomba serikali kuweka kanuni ambazo zitawezesha sheria ya watu wenye ulemavu namba tisa ya mwaka 2010.

Kanuni hiyo inaruhusu watu hao kupata matibabu bure na kuwapo wataalamu wa lugha ya alama katika vituo vya kutolea huduma za afya, ili kurahisisha mawasiliano kati yao na watoa huduma.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo kwa viongozi na watendaji wakiwamo wa idara ya afya na watu wenye ulemavu chini ya mradi wa kuondoa vikwazo kwa watu hao katika maeneo ya kutolea huduma za afya wenye thamani ya shilingi milioni 19 kutoka Shirika la The Foundation For Civil Society, mratibu wa mradi, Laurian Pankras, alisema sheria hiyo kutokuwa na kanuni ni kikwazo kikubwa kwao.

"Watu wenye ulemavu wakienda hospitalini wanatakiwa kulipa na bila fedha hawawezi kupata huduma na wakati mwingine wanaambiwa waende kwa wenyeviti wawape utambulisho, lakini kuna sheria, sera, matamko na maagizo mbalimbali ambayo hayafanyiwi kazi na kuwawezesha watu wenye ulemavu kutibiwa bure," alisema Pankras.

Naye Katibu wa Chama cha Watu wenye Ulemavu (CHAWATA) Mkoa wa Kagera kinachoratibu mradi huo, Sweetbert Mushanga, alisema watu hao wanakabiliwa na tatizo la kutokuwa na elimu ya ujasiriamali ambayo huwafanya washindwe kuunda vikundi ambavyo vingewawezesha kunufaika na mikopo inayotolewa na serikali kupitia halmashauri.

"Tunaishukuru serikali kwa kutukumbuka na kutenga asilimia mbili kutoka makusanyo ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya mikopo ya watu wenye ulemavu, lakini bado hatujanufaika ipasavyo kutokana na wengi kutokuwa na elimu ya ujasiriamali," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Muhaji Bushako, aliwataka watu wenye ulemavu kuweka viongozi wao hadi ngazi za vitongoji badala ya kuishia wilayani, ili wasaidie kubaini watoto walemavu waliofichwa majumbani, maana kuwa mlemavu hakuzuii mtoto kupata haki zake za msingi ikiwamo ya elimu.

# Agizo kurejeshwa milioni 320/- zilizotafunwa latolewa

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, ameiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kufikia Juni 30, iwe imekusanya fedha mbichi zote zaidi ya shilingi milioni 320 zilizoliwa na watendaji wa serikali baada ya kukusanya mapato.

Agizo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki katika baraza la madiwani kwa ajili ya kujadili hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema watendaji wa vijiji na mawakala wanaokusanya mapato ya serikali wamekula shilingi milioni 328, kitendo ambacho hakubaliani, na amemwagiza mkurugenzi wa halmashauri kuhakikisha fedha zote zinarudishwa kufikia Juni 30. "Sitaki kusikia kauli kuwa eti fedha hizo zimeliwa na watumishi pamoja na mawakala, watu wanafahamika walipo, hata kama halmashauri haijui namna ya kuwakamata wapeni kazi hiyo polisi ndani ya siku mbili watakuwa hapa na watalipa, sina mchezo na mapato ya serikali," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Dk. Khalfani Haule, alisema changamoto kubwa ni kuwa wanaokusanya mapato hayo wanakaa nayo muda mrefu badala ya kupeleka benki.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, baadhi ya watendaji wanakaa na fedha nyingi, siku moja nimemkuta mtendaji wa kijiji amekaa nyumbani kwake na shilingi milioni 70, fedha za makusanyo, kitendo ambacho ni hatari hata kwa usalama wake, alisema.

Alisema baadhi ya watendaji wamekuwa wakitumia kidogo kidogo fedha hizo na kujikuta wanadeni kubwa na wengine wanaiba fedha nyingi na kuamua kutoroka katika vituo vyao vya kazi na kukimbilia kusikojulikana.

Awali akifungua baraza hilo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Kalolo Ntila, alisema halmashauri inashindwa kufikia malengo ya makusanyo yake kutokana na baadhi ya watendaji ambao wamekuwa wakila fedha mbichi za makusanyo ya kodi.



Mmoja wa wanahisa wa Benki ya DCB na Waziri Mkuu wa zamani, Fredrick Sumaye (wapili kulia), akizungumza na Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Maharage Chande (wapili kushoto) wakati wa Mkutano Mkuu wa 19 wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki hiyo, uliofanyika na uzinduzi wa mwonekano mpya wa Benki ya Biashara ya DCB, Diamond Jubilee, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakazi Mkuranga walia kutofungiwa umeme

**Na Christina Mwakangale**

WAKAZI wa Kijiji cha Mlamleni, Kitongoji cha Bunguni 'B', Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wameelekeza kilio chao kwa Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, kuwatatulia kikwazo cha kutounganishiwa umeme kwenye eneo lao.

Wakazi hao wanalalamika kwamba kwa zaidi ya miaka miwili, wamekuwa wakituma maombi ya kuunganishiwa nishati hiyo bila mafanikio.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Dedan Hyera, akizungumza na Nipashe, alisema walipeleka maombi ya barua mwaka 2019 kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wilaya ya Mkuranga, ili kuunganishiwa umeme, bila ya mafanikio licha ya nguzo za umeme kupita mbele ya nyumba zao.

"Inashangaza, nguzo za umeme zipo mbele ya nyumba zetu, lakini umeme hatuna ndani, na hii barabara ni kubwa inatokea hadi wilayani, kila siku waziri anasema nguzo au umeme usipite jirani na nyumba bila kuwaunganishia wakazi.

"Kilichopo tunashuhudia umeme vitongoji vya wenzetu, vinavyotuzunguka mita 20 tu kutoka hapa Binguni 'B', kitongoji chetu kuna nyumba takribani 100 hatuna umeme," alisema Hyera.

Alisema kutokana na barua yao kutojibiwa mwaka 2019, waliandika kwa mara ya pili mwaka jana kukumbushia maombi yao, lakini hawajapatiwa umeme.

"Tunamwomba waziri asikie kilio chetu, kwani sisi tunakosa gani, simu, nguo, soda za baridi hatunywi, watoto hawasomi usiku, biashara jua likizama hakuna mvuto ni giza, sababu umeme hatuna. Tunatumia umeme wa nishati ya solar ya jua ambayo ni ghali kuunganisha mfumo wake nyumba nzima, inabidi uwe na shilingi 200,000 hadi milioni mbili," alisema Hyera.

Angelus Patory, mkazi wa eneo hilo, alisema Januari mwaka huu mtathmini kutoka shirika hilo, alipita kwenye eneo lao kutathmini na kwamba matarajio ya kupatikana umeme yangekuwa Machi, mwaka huu.

"Kila tunapokwenda TANESCO wilaya tunaambiwa tusubiri. Lakini mbona umeme umewafikia viongoji vingine eneo letu limerukwa?" alihoji Pastory.

Mwenyekiti wa Kitongoji Bunguni 'B', Michael Mgoli, aliiambia Nipashe kwamba analifahamu suala hilo na barua zilishaandikwa na kupelekwa TANESCO kuhusu suala hilo, lakini majibu yalikuwa ya mdomo.

"Tulijibiwa tusubiri mradi mwingine kwa sababu wa sasa zilipatikana nguzo 17 tu wakati zilihitajika pengine zaidi ya 100 kutosheleza. Wananchi walipisha mradi wa umeme uliopita mbele ya nyumba zao kwa kukata miti, mazao, lakini matokeo yake umeme haujaingia ndani ya nyumba," alisema Mgoli.

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Mkuranga, Theodory Shall, aliiambia Nipashe kwamba, wakazi wa eneo hilo wanapaswa kuwa na subira, kwa kuwa vipaumbele vya umeme ili kuwafikia wananchi huzingatia kwanza wilaya, kijiji, vitongoji na ujazilizaji.

Alisema serikali ina lengo kuyafikia maeneo yote ikiwamo vijiji na vitongoji kwa hatua kwa kuwa mahitaji ni makubwa, na kwamba wilaya hiyo ina vijiji 125 huku 71 vikifikiwa na 54 viko kwenye mchakato.

"Sula la umeme kupita mbele ya nyumba za wananchi na umeme hawaunganishwi inategemea umeme ni wa aina gani, kuna mkubwa na wa REA. Vijijini REA ndio mradi wao, hivyo wasubiri kufikiwa," alisema Theodory.

# TBS yafunguka kuhusu sababu wajasiriamali kukosa alama ubora

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI wengi wanakabiliwa na changamoto ya kukosa maeneo rasmi ya kufanya uzalishaji hali inayowafanya kuendesha shughuli za usindikaji wa bidhaa zao maeneo ya majumbani.

Kutokana na hali hiyo, Shirika la Viwango la Taifa (TBS) limesema ni vigumu kwao kupewa alama ya ubora.

Hayo yalisemwa na Mkaguzi wa TBS Kanda ya Kusini, Barnabas Jacob, alipokuwa akizungumza kuhusiana na zoezi la kuwatembelea wajasiriamali katika wilaya za Nyasa na Mbada na kuwapa elimu kuhusu kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

Kwa mujibu wa Jacob, wilaya hizo zina wajasiriamali wanaozalisha bidhaa mbalimbali zinazothibitishwa na shirika hilo ambapo wamebaini wengi wanafanya shughuli za usindikaji wa bidhaa za chakula na vipodozi katika maeneo ambayo sio rasmi.

Kwa mujibu wa Jacob, changamoto hiyo inasababishwa na sababu mbalimbali, lakini kubwa ambayo wameiona ni ukosefu wa mitaji ya kutenga au kujenga maeneo ya usindikaji.

"Changamoto nyingine ni kwamba baadhi ya halmashauri haziwapi kipaumbele wajasiriamali kwa kuwasaidia kuwajengea vizimba vya usindikaji na hata mikopo wanayopewa kwa ajili ya mitaji ni midogo, kwani unakuta mtu anapewa Sh. milioni moja au mbili ambazo hazitoshelezi hata kujenga chumba kimoja kwa ajili ya uzalishaji," alisema Jacob.

Alisema ni muhimu kwa kila halmashauri kuwapa kipaumbele wajasiriamali kwa kuhakikisha wanawajengea vizimba kwa ajili ya uzalishaji na kuwawezesha na mitaji kidogo ili iwe rahisi kwa TBS kuthibitisha bidhaa zao, kwani itakuwa rahisi kuwa na maeneo anayofanyia shughuli zao.

Alitoa mfano kwa Halmashauri ya Wilaya Mbinga, akisema yenyewe inasaidia vikundi vya wajasiriamali mitaji mikubwa kuanzia milioni 10 hadi 20.

"Hiyo mitaji inawasaidia kujenja jengo na kununua mashine au vifaa vya kufanya usindikaji," alisema Jacob na kutoa wito kwa halmashauri zingine kuiga mfano huo kwa kuwapa kipaumbele wajasiriamali.

## Serikali yafungua mnada uliofungwa miaka 20

**Na Mbaraka Kambona,** MARA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameielekeza Halmashauri ya Mji wa Tarime kuufungua mnada wa mpakani wa Magena uliofungwa kwa zaidi ya miaka 20 ili uanze kufanyakazi ya biashara ya mifugo kama ilivyokusudiwa hapo awali.

Waziri Ndaki alitoa agizo hilo wakati wa ziara yake ya siku moja aliyoifanya mkoani Mara mwishoni mwa wiki, alipotembelea kuona hali ya mnada huo na kuruhusu uanze kufanya kazi baada ya kuelezwa na kujiridhisha kuwa sababu zilizosababisha mnada huo kufungwa hazipo tena.

"Leo nimekuja kuufungua mnada huu wa Magena uanze kufanya kazi mara moja, ninaelekeza kuwa Halmashauri ya Mji wa Tarime na watendaji katika ngazi ya wizara yangu wakutane haraka ili wapange siku ambayo mnada huu utaanza kufanyakazi, na hiyo taarifa nipewe ndani ya wiki moja," alisema Ndaki.

Alisema serikali imedhamiria kuufanya mnada huo kuwa wa kimataifa na watahakikisha wanaboresha miundombinu yote iliyochakaa ili iweze kutoa huduma nzuri na serikali ianze kukusanya mapato yake.

"Kwa kuanzia tumetenga Sh. milioni 150 kwa ajili ya kuanza kuboresha miundombinu ya mnada huu na tutaendelea kuuboresha zaidi ili uweze kuvutia watu wengi wakiwemo kutoka nchi za jirani kuja kufanya biashara hapa," alisema Ndaki.

Aidha, aliwataka wananchi wa Wilaya ya Tarime, hususan wanaoishi katika Kijiji cha Magena, kuhakikisha wanautunza mnada huo ili uweze kuwa na tija kwao pamoja na nchi kwa ujumla.

Aliwaonya wenye tabia ya wizi wa mifugo kuacha vitendo hivyo kwa kuwa ndiyo vilichangia mnada huo kufungwa, na kwamba serikali ipo imara na imejipanga kuhakikisha wanakomesha vitendo hivyo ili wafanyabiashara wa mifugo waweze kuutumia mnada huo na kufanya shughuli zao kwa amani.

"Serikali imedhamiria kuboresha maisha ya wananchi wake, kufunguliwa kwa mnada huu ni katika jitihada za kuboresha maisha yenu ili kila mmoja aweze kupata maendeleo yake kupitia shughuli halali anazozifanya," alifafanua Ndaki.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ambaye ni Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, alisema kufunguliwa kwa mnada huo kutatoa fursa kwa wananchi wa mkoa huo kujiongezea kipato kupitia shughuli mbalimbali zitakazokuwa zinaendelea katika mnada huo.

"Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwa kutufungulia mnada huu, lakini nakuomba usiishie kuwa mnada wa mpakani tu, ni muhimu tukauboresha kwa kujenga miundombinu ya kisasa ili uwe wa kimataifa na serikali iweze kukusanya mapato mazuri na wananchi pia waweze kufaidika kupitia rasilimali zao," alisema Waitara.

Alisema ni muhimu operesheni inayoendeshwa na Jeshi la Polisi nchini ya kupambana na wizi itumike pia kushughulika na wezi wa mifugo ili biashara hiyo iweze kwenda vizuri na kushamiri mkoani humo.

Mnada huo ulikuwa kati ya minada 10 ya mipakani na ulijengwa mwaka 1995 na kufunguliwa mwaka 1996 na kufanya kazi kwa mwaka mmoja kabla ya kufungwa kwa sababu zilizotajwa ikiwamo wizi wa mifugo na sababu nyingine za kiusalama na kusababisha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo kuufunga Mei 14, 1997.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

# Bajeti Nishati yaainisha mafanikio lukuki sekta ya umeme

- **Watanzania milioni 47 sasa waunganishwa na umeme**



*Mkurugenzi Mtendaji wa Tanesco, Dk. Tito Mwinuka*

**Na Joseph Mwendapole**

KATIKA utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021 Wizara hiyo imeainisha mafanikio mengi yaliyofikiwa mpaka sasa kwa wananchi wengi kupata huduma ya umeme tena kwa gharama nafuu.

Hayo yamo kwenye Hotuba ya Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, wakati alipowasilisha Makadirio ya Mapato, Matumizi na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2020/21 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2021/22. Miongoni mwa mafanikio yaliyoainishwa na Wizara hiyo kwenye sekta ya nishati ni kutokana na utekelezaji wa maeneo hayo ya kipaumbele ambayo ni pamoja na kuendelea na Ujenzi wa Mradi wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) MW 2,115 ambao hadi kufikia mwezi Mei, 2021 utekelezaji wake kwa ujumla umefikia asilimia 52.

Waziri Kalemani alisema serikali imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Rusumo MW 80 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 80 na kuanza maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya kufua umeme ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222); Alitaja mafaniko mengine kuwa ni kukamilika kwa Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme msongo wa kV 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita yenye urefu wa kilomita 55 ambao ulikamilika mwezi Septemba, 2020 na kuunganisha umeme vijiji takriban 10 katika Wilaya ya Geita vinavyopitiwa na mradi huo.

Alitaka maendeleo mengine kuwa ni kukamilika kwa ujenzi wa Mradi wa Njia ya Kuendesha Treni ya Kisasa ya Mwendokasi ya kutumia umeme (Standard Gauge Railway - SGR) awamu ya kwanza yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Dar es Salaam hadi Kingolwira, Morogoro ilikamilika mwezi Septemba, 2020 kwa gharama ya Shilingi bilioni 76.26 kwa fedha za ndani kwa asilimia 100.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni kukamilika kwa mradi huu kutaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kuanza kuendesha treni ya kisasa ya mwendokasi ya kutumia umeme katika nchi za Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa Dk. Kalemani mafanikio mengine ni kuendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya vijiji 10,312 vimeunganishiwa umeme ikilinganishwa na vijiji 2,018 vilivyokuwa vimeunganishwa umeme mwaka 2015 sawa na ongezeko la vijiji 8,294 sawa na asilimia 86 ya vijiji vya Tanzania Bara vimepata umeme;

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni kuendelea kuhamasisha na kusisitiza uzalishaji wa vifaa vya kujenga miradi ya umeme nchini na kuzuia uingizaji wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya umeme ikiwemo nguzo, mashineumba (transfoma), nyaya na mita za LUKU ndani ya nchi na hivyo kurahisisha upatikanaji wa vifaa hivyo na kuokoa takriban Shilingi bilioni 162.23.

Alisema uzalishaji huo pia umechangia ongezeko la ajira nchini ambapo takriban Watanzania wapatao 22,820 wameajiriwa katika viwanda hivyo kati ya mwaka 2017 hadi sasa.

Alisema serikali imeendelea kuunganisha umeme wateja wapya nchini kwa kasi ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya Watanzania wanaonufaika na huduma ya umeme wamefikia takriban milioni 47 sawa na asilimia 78 ya Watanzania wapatao milioni 60.

Waziri alisema serikali imeendelea kuondoa hasara za Shirika la TANESCO zilizokuwepo za Shilingi bilioni 349 katika kipindi cha miaka 2015-2017. Hasara hizi, pamoja na mambo mengine zilizotokana na kutumia mafuta mazito na kuagiza vifaa kutoka nje ya nchi.

Dk. Kalemani aliendelea kusema kuwa serikali imezidi kuondoa gharama kubwa wanazotozwa wananchi wa kawaida za kuuziwa umeme na wazalishaji wadogo kutoka Shilingi 3,500 au zaidi kwa uniti moja ya umeme hadi Shilingi 100 kwa uniti kama inavyotozwa na TANESCO.

Utekelezaji wa agizo hili ulianza mwaka 2019/20. Mafanikio mengine aliyataja kuwa ni kuendelea kuongezeka kwa mapato ya Shirika la TANESCO kutoka wastani wa Shilingi bilioni 72 kwa mwezi mwaka 2016 kufikia wastani wa Shilingi bilioni 160 kwa mwezi mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la takriban asilimia 102 akiongeza kuwa ongezeko hilo pia limetokana na kutumia mfumo wa LUKU wa kulipa ankara za umeme kwa wateja wote nchini; Waziri Kalemani aliliambia Bunge kuwa serikali imeendelea kuongeza kasi ya kufuatilia madeni sugu ya wateja wa TANESCO na kupungua kwa madeni haya kutoka Shilingi bilioni 272 mwaka 2017 kufikia Shilingi bilioni 48.9 mwaka 2020.

Aidha, alisema Shirika la TANESCO limeendelea kujitegemea na kuendesha shughuli zake bila kupata ruzuku ya takriban Shilingi bilioni 143 kwa mwaka kutoka Serikalini.



*Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani*

Kwa mujibu wa Waziri Kalemani, Serikali kupitia TANESCO na REA imeendelea kuunganisha umeme kwa Shilingi 27,000 katika maeneo yote ya vijijini ikiwa ni pamoja na Mitaa katika Majiji na Manispaa (Vijiji Miji) kulingana na Mpango wa Kupeleka Umeme Vijijini; tofauti na ilivyokuwa huko nyuma ambapo wateja wa aina hii walikuwa wanaunganishwa kwa Shilingi 177,000 au zaidi.

Alisema serikali imeendelea kuongeza matumizi ya nguzo za zege katika kujenga njia za kusafirisha umeme katika baadhi ya maeneo yenye mahitaji hayo na viwanda vya ndani vya kuzalisha nguzo za zege vimeongezeka kutoka kimoja mwaka 2018 na kufikia vitano (5) vinavyozalisha zaidi ya nguzo 15,000 kwa mwaka.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni kukamilika kwa majadiliano na kusainiwa kwa Mkataba kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji (Host Government Agreement - HGA), Mkataba wa Ubia (Shareholding Agreement - SHA) na kuanza taratibu za ujenzi wa mradi wa EACOP.

Alisema mafanikio mengine kuwa ni kupungua kwa matumizi ya mafuta ya taa, hususan vijijini kutoka lita milioni 1 kwa mwezi mwaka 2016/17 hadi lita laki 4.5 mwaka 2020/21 kutokana na kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme vijijini.

Waziri Kalemani alisema katika utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2020/2021 mafanikio yaliyopatikana yalikuwa ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo Julius Nyerere MW 2,115, Rusumo MW 80, Kinyerezi I Extention MW 185, Ruhudji MW 358, Rumakali MW 222, Malagalasi MW 49.5, Umeme wa Jua MW 150, Umeme wa Upepo MW 200 na Joto Ardhi MW200.

Alitaja mpango mwingine uliokuwa kwenye bajeti ya 2020/21 kuwa ni kuzalisha umeme kwa kutumia makaa yam awe WM 600, ujenzi wa njia za kusafirisha umeme ikiwemo Singida-Arusha Namanga KV 400, North West Grid Exention Mbeya-Sumbawanga -Mpanda-Kigoma-Nyakanazi KV 400.

Kwa mujibu wa Dk. Kalemani mpango mwingine ulikuwa ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rufiji-Chalinze-Dodoma- KV 400, Chalinze-Kinyerezi KV 400, Geita-Nyakanazi KV 220, Rusumo -Nyakanazi KV 220, Bulyankulu-Geita KV 220, Tabora-Kigoma KV 132, Tabora-Katavi KV 132, Ibadakuli- Imalilo KV 220 na kuendelea na awamu ya tatu ya mradi kabambe wa kupeleka umeme vijijini.

TOLEO MAALUM

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

# Upatikanaji umeme waendelea kuimarika

## * Bei sasa kushuka, Tanzania kuuza umeme nje

Na Joseph Mwendapole

KATIKA bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 serikali imeelezea kuridhishwa na hali ya upatikanaji wa umeme kwenye maeneo yote nchini na bei ya nishati hiyo inatarajiwa kushuka miradi ya kimkakati itakapokamilika na kuanza uzalishaji.

Hayo yamo kwenye Hotuba ya Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, wakati alipowasilisha Makadirio ya Mapato, Matumizi na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2020/21 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2021/22.

Alipozungumzia sekta ndogo ya umeme, Waziri Kalemani alisema hali ya upatikanaji umeme nchini imeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa ilifikia MW 1,573.65 kati ya hizo MW 573.70 zinatokana na vyanzo vya maji, MW 901.32 gesi asilia na MW 10.50 tungamotaka (Biomass).

Aliliambia Bunge kuwa uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO ambayo huchangia asilimia 86.57 na mitambo ya wazalishaji binafsi (IPP/SPPs) ambayo huchangia asilimia 13.43.

Alisema TANESCO inamiliki mitambo ambayo haijaunganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa yenye uwezo wa kuzalisha MW 32.21 na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini kufikia MW 1,605.86.

Waziri alisema mahitaji ya juu ya umeme yameendelea kuongezeka na kufikia MW 1,183.28 sawa na ongezeko la asilimia 2.75 ikilinganishwa na MW 1,151.66 ya mwaka 2019/20.

Kwa mujibu wa Dk. Kalemani hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya urefu wa njia za kusafirisha umeme umefikia kilomita 6,111.27 sawa na ongezeko la asilima 25.94, ikilinganishwa na kilomita 4,852.7 za mwaka 2015/16.

Alisema kati ya hizo, njia za msongo wa kV 400 ni kilomita 670, kV 220 ni kilomita 3,225.7, kV 132 ni kilomita 1,672.57 na kV 66 ni kilomita 543. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021

miundombinu ya usambazaji umeme imeendelea kuongezeka na kufikia jumla ya kilomita 147,156.80 sawa na ongezeko la asilimia 139.77 ikilinganishwa na kilomita 61,373.76 zilizokuwa zimefikiwa mwezi Juni, 2015.

Alisema kati ya hizo, njia za msongo wa kV 33 ni kilomita 47,106.07, msongo wa kV 11 ni kilomita 12,457.21 na msongo wa kV0.4 ni kilomita 87,593.52.

Kuhusu miradi ya umeme, Dk. Kalemani alitaja Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere ambao ukikamilika utazalisha MW 2,115 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji.

Alisema gharama za mradi huo ni Shilingi trilioni 6.55 zinazotolewa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100.

Waziri alisema katika mwaka 2020/21, kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha uchimbaji na ujenzi wa handaki la kuchepusha maji ya Mto Rufiji (diversion tunnel), kuendelea na ujenzi wa bwawa (main dam and spillways), ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (tunnels), ujenzi wa kituo cha kuzalishia umeme (Power House) na ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (Switch yard).

Alisema hadi kufikia mwezi Mei, 2021, jumla ya Shilingi trilioni 2.495 zimelipwa kwa mkandarasi sawa na asilimia 100 ya fedha iliyotakiwa kulipwa kulingana na hatua ya utekelezaji wa mradi iliyofikiwa.

Kwa mujibu wa Dk. Kalemani kwa ujumla utekelezaji wa mradi katika maeneo muhimu matano (critical path) hadi kufikia mwezi Mei, 2021 umefikia wastani wa asilimia 52 na hadi sasa jumla ya wafanyakazi 7,243 wameajiriwa na kati ya wafanyakazi hao 6,452 ni Watanzania sawa na asilimia 89.1 na kutoka nje ya nchi ni 791 sawa na asilimia 10.9.

Waziri Kalemani alisema katika kipindi cha mwaka 2021/22, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuendelea na kukamilisha ujenzi wa bwawa (main dam and spillways), ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (tunnels), ujenzi wa kituo cha kuzalishia umeme (Power House) na ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (Switch yard).

Alisema jumla ya Shilingi trilioni 1.4 fedha za ndani zimetengwa katika mwaka 2021/22 kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo na kwamba ujenzi wa mradi huo



Mitambo ya kuzalisha umeme

ulianza mwezi Juni, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022.

Aidha, alisema kukamilika kwa mradi huo pamoja na miradi mingine kutafanya nchi kuwa na jumla ya takriban MW 5,000 kufikia mwaka 2025 na katika kipindi hicho mahitaji yetu ya juu ya umeme yanatarajiwa kufikia MW 2,677 hivyo kuwa na ziada ya takriban MW 2,323 na kuweza kuuza umeme nje ya nchi na kuongeza mapato ya Shirika.

Aidha, alisema Serikali itaweza kutekeleza azma yake ya kupunguza bei za umeme kwa wananchi.

Kuhusu Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Ruhudji - MW 358, alisema mradi huo unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 358 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji na njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 170 kutoka Ruhudji mkoani Njombe hadi kituo cha kupoza umeme cha Kisada mkoani Iringa.

Alisema gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 407.4 sawa na takriban Shilingi bilioni 958.25 na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 unaokadiriwa kugharimu Dola za Marekani milioni 53.2 sawa na takriban Shilingi bilioni125.13.

Alisema katika mwaka 2020/21, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kuhuisha Upembuzi Yakinifu (Update of Feasibility Study) wa mradi na kuandaa zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kujenga mradi.

Alieleza kuwa katika mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni pamoja na kusaini mkataba wa ujenzi na kuanza ujenzi wa mradi na jumla ya Shilingi bilioni 65.60 zimetengwa katika mwaka 2021/22 ili kutekeleza kazi hizo na kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 45.00 ni fedha

za ndani na Shilingi bilioni 20.60 ni fedha za nje.

Alisema ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2021 na kukamilika mwezi Julai, 2024.

Kuhusu Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rumakali - MW 222, Waziri alisema mradi huo unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 222 kwa kutumia maji ya Mto Rumakali mkoani Njombe na njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 150 kutoka katika mitambo hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo mkoani Mbeya.

"Gharama za mradi huu kwa pamoja zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni

388.22 sawa na takriban Shilingi bilioni 913.14," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Kalemani katika mwaka 2020/21, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kuhuisha Upembuzi Yakinifu wa mradi na kuandaa makabrasha ya kumpata mkandarasi wa kujenga mradi.

Alisema kwa mwaka 2021/22, Wizara ya Nishati itaendelea kutekeleza vipaumbele mbalimbali vikiwemo kuongeza uzalishaji wa umeme nchini kufikia MW 5,000 katika kipindi cha miaka mitano (5) ijayo kwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo miradi mikubwa ya kimkakati na ya kielelezo .

Alitaja miradi hiyo kuwa ni ya Julius Nyerere (MW 2,115), Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222) pamoja na miradi mingine ya Kinyerezi I - Extension (MW 185), Rusumo (MW 80), Malagarasi (MW 49), Mtwara (MW 300) na Somanga Fungu (MW 330).

Alisema pamoja na miradi hiyo ya uzalishaji umeme, Serikali pia itaendelea kutekeleza miradi ya kuimarisha mifumo ya usafirishaji umeme nchini kwa kutekeleza miradi mbalimbali.

Waziri Kalemani aliliambia Bunge kuwa miradi hiyo ni mradi wa kusafirisha umeme wa North - West Grid Extension kV 400; Singida - Arusha - Namanga kV 400; Rufiji - Chalinze - Dodoma kV 400; Chalinze - Kinyerezi kV 400; Rusumo - Nyakanazi kV 220, Geita - Nyakanazi kV 220; Ibadakuli (Shinyanga) - Imalilo (Simiyu) kV 220; Tabora - Kigoma kV 132; na Tabora - Katavi

kV 132, pamoja na vituo vya kupoza umeme vya Handeni na Kilindi mkoani Tanga.

Alisema, pamoja na maeneo hayo ya kisekta, Wizara pia itazingatia maeneo mengine yanayolenga kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi zake katika kusimamia Sekta, kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi ili kutoa huduma bora; na kuendelea kuelimisha umma kuhusu masuala ya nishati.




Bwawa la kuzalisha umeme la JNHPP Rufiji

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

# Umeme wasambazwa kwa kasi vijijini

## • Vijiji 10,312 vyapatiwa umeme nchi nzima

**Na Mwandishi Wetu**

Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi chake Afrika zilizofanikiwa kuwaunganishia nishati ya umeme wananchi wake wengi wa maeneo ya vijijini kwani hadi sasa vijiji 10,312 vimefikiwa.

Hayo yamo kwenye Hotuba ya Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, wakati alipowasilisha Makadirio ya Mapato, Matumizi na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2020/21 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2021/22.

Kwenye hotuba yake ya bajeti, Waziri Kalemani alisema Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu ulilenga kufikisha umeme katika vijiji 7,873 na hadi kufikia Desemba 2015, jumla ya vijiji 2,018 vilikuwa vimefikiwa na huduma ya umeme na kwamba idadi hiyo imeongezeka na kufikia vijiji 10,312 mwezi Mei, 2021 sawa na ongezeko la vijiji 8,294.

Alisema hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme ni 1,956 sawa na asilimia 14 ya vijiji vyote 12,268 vya Tanzania Bara na vitapelekewa umeme kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ambao unaendelea kutekelezwa na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2022.

Kwa mujibu wa Dk. Kalemani kukamilika kwa mradi huo kutafanya vijiji vyote 12,268 vya Tanzania Bara kufikiwa na umeme.

Alisema kazi zilizofanyika katika mwaka 2020/21 ni pamoja na kukamilisha Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza, kuendelea kusambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa miji (Peri Urban) katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, kukamilisha usambazaji umeme katika vitongoji vilivyopitiwa na miundombinu ya usambazaji umeme wa msongo wa kati kupitia Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Kwanza katika mikoa nane.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni kuanza kwa usambazaji umeme katika vitongoji vilivyopitiwa na miundombinu ya usambazaji umeme wa msongo wa kati kupitia Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili katika mikoa 25.

Alisema wameendelea kuunganisha wananchi kwa kutumia mifumo ya nishati jadidifu katika maeneo yaliyopo mbali na Gridi



*Waziri wa Nishati Medard Kalemani akizungumza na mnufaika wa umeme vijijini*

zikiwemo Taasisi za Umma katika visiwa vilivyopo katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Delta ya Rufiji.

Alisema katika kipindi cha kuanzia mwezi Aprili, 2020 hadi kufikia mwezi Aprili, 2021, jumla ya Taasisi 18,844 zimeunganishiwa umeme na hivyo kufanya jumla ya Taasisi zilizounganishiwa umeme kufikia 28,044 sawa na ongezeko la asilimia 84.5.

Waziri alisema Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu - Mzunguko wa Kwanza (REA III - Round I), ulilenga kupeleka umeme katika vijiji 3,559 na kuunganisha wateja wa awali 180,768.

Alisema utekelezaji wa mradi huo pia ulihusisha kupeleka umeme katika vitongoji 419 ambavyo vina Taasisi zinazotoa huduma kwa jamii zikiwemo Taasisi za Afya na Elimu ndani ya vijiji vilivyofikiwa na umeme, na hivyo kupelekea wateja wa awali kuongezeka hadi kufikia 227,561.

Alisema gharama ya mradi ni Shilingi trilioni 1.157. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya vijiji 3,378 kati ya 3,559 sawa na asilimia 94.9 na vitongoji 317 kati ya 419 sawa na asilimia 75.7 vilipelekewa umeme na kuunganisha jumla ya wateja 162,198 kati ya 227,561 sawa na asilimia 71.3.

Alisema Mradi ulianza mwezi Julai, 2018 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021.

Kuhusu Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu - Mzunguko wa Pili (REA III - Round II), Waziri alisema mradi huu unalenga kupeleka umeme katika vijiji 1,956 ambavyo havijafikiwa na umeme na hivyo kukamilisha kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vyote 12,268 vya Tanzania Bara.

Vilevile, Waziri alisema mradi unahusisha kupeleka umeme katika vitongoji 1,492 na gharama za mradi ni Shilingi trilioni 1.24 na unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100.

Alisema Mradi huu ulizinduliwa rasmi kitaifa tarehe 15 Machi, 2021 na katika mwaka 2021/22 Shilingi bilioni 181.99 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Miradi ya Ujazilizi Katika Vitongoji Mzunguko wa Pili (Densification II), Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili A (Densification IIA), Waziri alisema mradi huo unalenga kupeleka umeme katika vitongoji ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme katika mikoa tisa (9) ambayo ni Dodoma, Singida, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Kilimanjaro, Mbeya, Pwani na Tanga.

Alisema mradi huo utahusisha kupeleka umeme katika vitongoji 1,103 na kuunganisha jumla ya wateja wa awali 69,079 na gharama ya mradi ni Shilingi bilioni 117.02 ambao ulizinduliwa rasmi kitaifa tarehe 24 Septemba, 2020.

Aidha, alisema utekelezaji wa mradi ulianza mwezi Agosti, 2020 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021.

Kuhusu Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili B (Densification IIB), Waziri alisema mradi huu unalenga kupeleka umeme katika vitongoji 1,686 na kuunganisha jumla ya wateja wa awali 95,334 katika mikoa kumi (10) ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe, Simiyu na Songwe na gharama ya mradi inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 249.3 na unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa.

Kwa mujibu wa Waziri Kalemani Mradi huo upo katika hatua za kuwapata makandarasi na unatarajiwa kuanza mwezi Septemba 2021 na utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 12.

Alizungumzia Miradi ya Kusambaza Umeme katika Maeneo Yaliyo Pembezoni mwa Miji (Vijiji Miji) - Peri Urban, ambapo alisema, mradi wa Peri - Urban unalenga kusambaza umeme katika maeneo, vitongoji na mitaa iliyopo pembezoni mwa miji (vijiji miji) yenye uhitaji mkubwa wa umeme na maeneo hayo yanashabihiana na maeneo ya vijijini.

Waziri alisema Mradi wa Peri Urban katika Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kigamboni unahusisha kusambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa miji (vijiji miji) katika Wilaya zote za Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kigamboni mkoa wa Dar es Salaam, ambapo maeneo 216 yalipangwa kupatiwa umeme na kuunganisha wateja wa awali 37,713 kwa gharama ya Shilingi bilioni 80.5 na unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania.

"Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021, jumla ya maeneo 214 kati ya 216 yamefikishiwa umeme sawa na asilimia 99.1 na kuunganisha wateja wa awali 28,875 kati ya 37,713 sawa na asilimia 76.6. Utekelezaji wa mradi ulianza mwezi Novemba, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2021," alisema.

Kuhusu Mradi wa Peri Urban katika Mikoa ya Arusha, Dodoma na Mwanza, Waziri alisema mradi huo umelenga kusambaza umeme katika maeneo ya pembezoni mwa miji kwa mikoa ya Dodoma, Mwanza na Arusha ambapo maeneo 160 yamepangwa kupatiwa umeme na kuunganisha wateja wa awali 16,328, gharama ya mradi ikiwa ni Shilingi billion 31.34 nma ulianza mwezi Mei, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2022.

Kuhusu Miradi wa Kusambaza Umeme Unaotokana na Nishati Jadidifu katika Maeneo Yaliyo Nje ya Gridi ya Taifa (Off - Grid Projects), alisema mradi huu unalenga kutumia vyanzo vya nishati jadidifu kupeleka umeme katika vijiji vilivyopo katika maeneo yaliyo nje ya Gridi ya Taifa ambapo vijiji 119 vitanufaika kupitia mradi huu.

Alisema Vijiji hivyo vinahusisha pia Visiwa vyote ambavyo havijafikiwa na huduma za umeme na Mradi unatekelezwa kupitia utaratibu wa Ufadhili wa Malipo kwa Matokeo (Results Based Financing - RBF) na unalenga kukuza Sekta Binafsi katika kutekeleza miradi ya nishati jadidifu kwa maeneo yaliyo nje ya gridi ya Taifa.

Alisema gharama ya mradi ni Dola za Marekani milioni 18 sawa na takriban Shilingi bilioni 42.34 na unafadhiliwa na nchi za Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo (Sida) na Uingereza kupitia Shirika lake la Maendeleo (DFID).

Kwa mujibu wa Waziri Kalemani hadi kufikia mwezi Aprili, 2021, Serikali kupitia REA ilifadhili miradi 13 yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa jumla ya MW 9.635 kwa kutoa ruzuku ya Dola za Marekani milioni 10.07 sawa na takriban Shilingi bilioni ambapo ambapo jumla ya vijiji 108 kati ya 119 sawa na asilimia 90.7 vilipatiwa umeme na kuunganisha wateja wa awali 18,023 kati ya 20,020 sawa na asilimia 90.

TOLEO MAALUM

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

# Mpango kabambe uzalishaji na matumizi gesi asilia

## * Futi za Ujazo trilioni 19.7 kutumika

**Na Joseph Mwendaple**



*Baadhi ya mitambo ya kuzalishia umeme*

KATIKA Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 serikali imeweka mikakati kabambe ya kuinua uzalishaji na matumizi ya gesi asilia kama ilivyosomwa kwenye bajeti ya Wizara ya Nishati bungeni jijini Dodoma.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani alipokuwa anawasilisha bajeti yake aliliambia Bunge kuwa Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia (NGUMP).

Alisema mpango huo ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 na kwamba Katika Mpango huo, jumla ya Futi za Ujazo Trilioni 19.7 za gesi asilia zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani katika uzalishaji wa umeme, viwandani, majumbani, taasisi na magari.

Alisema katika kutekeleza mpango huo, Serikali imeendelea kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia JICA kuandaa Mpango wa Kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia Nchini (Domestic Natural Gas Promotion Plan - DNGPP).

" Mpango huu unalenga zaidi usafirishaji wa gesi asilia kwenda maeneo mbalimbali nchini pamoja na kuainisha matumizi ya teknolojia nafuu katika usambazaji wa gesi asilia," alisema.

Alisema katika mwaka 2020/21 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha Mpango wa Kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia Nchini (Draft Domestic Natural Gas Promotion Plan - DNGPP) na kukusanya taarifa na kupitia stadi mbalimbali kwa ajili ya uhakiki wa mahitaji ya gesi asilia nchini.

Alisema katika mwaka 2021/22 kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuhuisha Mpango na kukamilisha DNGPP; kufanya upembuzi yakinifu wa kina wa teknolojia kwa mujibu wa Mpango wa DNGPP, kuhakiki mahitaji ya gesi asilia nchini na kuanza hatua za awali za utekelezaji Mradi wa mfano katika Jiji la Dodoma.

Kuhusu miradi ya kusafirisha mafuta, Waziri alisema Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania mradi huu unahusu ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi (crude oil) kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga nchini Tanzania.

Alisema lengo la mradi huu ni kusafirisha mafuta hayo kwenda katika Soko la Kimataifa,gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani bilioni 3.558 sawa na takriban Shilingi trilioni 8.369.

Aidha, alisema kazi zilizotekelezwa hadi mwezi Mei, 2021 ni pamoja na kukamilisha majadiliano na kusainiwa kwa mkataba kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji (Host Government Agreement - HGA) na Mkataba wa Ubia (Shareholding Agreement - SHA) kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji.

Aidha, alisema majadiliano yamekamilika na kuridhiwa kusainiwa (intialed) kwa mikataba ya uendeshaji wa Bandari ya Chongoleani na mikataba ya ukodishaji wa ardhi kwa ajili ya mkuza na maeneo ya kipaumbele ya mradi na kukamilisha taratibu za kuanza kulipa fidia kwa Wananchi wa maeneo hayo.

Aidha, alisema katika mwaka 2021/22, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu utekelezaji wa mradi na fursa zilizopo; na kusimamia ujenzi wa mradi pamoja na wawekezaji wengine.

"Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa kazi hizo na ujenzi wa mradi umeanza mwezi Mei, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024," alisema.

Kuhusu uhifadhi na Biashara ya Mafuta, alisema Serikali kupitia TPDC imeendelea na utekelezaji wa kuanzisha na kusimamia Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta ya Akiba ya Dharura (Strategic Petroleum Reserve - SPR) na TPDC inamiliki maeneo yanayotazamiwa kujengwa maghala ya kuhifadhia mafuta (Tank Farms) katika mikoa ya Shinyanga (Isaka), Katavi (Mpanda), Njombe (Makambako), Uyole (Mbeya) na Kigoma hadi kufikia mwezi Machi 2021.

Alisema TPDC imekamilisha utwaaji wa ardhi katika mikoa ya Dodoma (Zuzu), Tanga (Chongoleani) na imeendelea na taratibu za utwaaji ardhi Mkoa wa Dar es Salaam (Kigamboni) na TPDC itajenga maghala ya kuhifadhia mafuta ya ujazo tofauti kulingana na ukubwa wa eneo kuanzia tani 45,000 hadi 100,000.

Alisema TPDC imeanza kufanya biashara ya uagizaji na uuzaji wa mafuta ambapo hadi kufikia mwezi Mei, 2021 shehena nane (8) za mafuta zenye jumla ya ujazo wa takriban tani 8,253 zimepokelewa katika Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema katika mwaka 2021/22, Serikali kupitia TPDC itaendelea na biashara ya uagizaji na uuzaji wa mafuta kwa ujazo usiopungua tani 2,000 kwa mwezi na kiwango hiki kitaendelea kuongezeka na kwamba Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya Shilingi bilioni 47.95 kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa mafuta (oil cargo stock).

Kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi (Refined Petroleum Products) kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia), alisema mradi huo unahusu ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es Salaam hadi Zambia lenye urefu wa takribani kilomita 1,710 likiwa na matoleo ya mafuta (take-off points) katika maeneo ya Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe.

Aidha, Waziri alisema Bomba hilo litajengwa katika mkuza wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la TAZAMA na litamilikiwa na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Zambia na Kukamilisha hadidu za rejea za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa Mradi zimeandaliwa na Kamati ya Pamoja ya Wataalamu wa nchi zote mbili (JTC).

Waziri alisema katika kipindi cha mwaka 2021/22 kazi zitakazofanyika ni pamoja na kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi pamoja na kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii na jumla ya Shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa kugharamia kazi zilizopangwa.

Akizungumzia udhibiti wa shughuli za mkondo wa juu wa mafuta na gesi asilia, alisema katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia PURA imekamilisha uhakiki na ukaguzi wa gharama za uwekezaji na mapato yatokanayo na uzalishaji wa gesi asilia kwa mwaka 2019 na 2020 na kuokoa jumla ya Shilingi bilioni 26.45 na hivyo kuongeza pato la Serikali katika mgao wake wa uuzaji gesi asilia.

Alisema kwa mwaka 2021/22 Serikali kupitia PURA itasimamia uchorongaji wa kisima kimoja cha utafutaji (Chikumbi-1) katika kitalu cha Ruvuma, kisima kimoja (1) cha utafutaji (Mruka-1) na kisima kimoja (1) cha uendelezaji (Mambakofi-2) katika kitalu cha Ruvu; na kisima kimoja (1) cha utafutaji (Tausi-1) katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini.

Aidha, alisema PURA itaendelea na ukaguzi katika maeneo yote ya utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia nchini. Katika mwaka 2021/22, Serikali imetenga Shilingi bilioni 1.69 fedha za ndani ili kuwezesha shughuli za udhibiti za mkondo wa juu wa Petroli.

Kuhusu hali ya upatikanaji wa bidhaa za petrol nchini, alisema hali ya upatikanaji wa mafuta nchini imeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka na kwa mwaka 2020/21, hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya matumizi ya hapa nchini ni lita bilioni 3.14 ikilinganishwa na lita bilioni 3.11 zilizoingizwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 1.14.

Alisema kiasi cha mafuta kilichoingia hapa nchini kwa ajili ya nchi jirani (Transit products) mwaka 2020/21, hadi kufikia mwezi Aprili 2021 ni lita bilioni 2.23 ikilinganishwa na lita bilioni 2.06 zilizoingizwa mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia 8.3.

Alisema Serikali imeendelea kuimarisha udhibiti katika upokeaji wa mafuta kutoka katika meli kwa kufunga flowmeter za teknolojia ya kisasa inayotumika kupima bidhaa za mafuta ya petroli yanayoshushwa ili kupata kodi na tozo stahiki.

"Serikali kupitia EWURA imeelekeza kampuni zinazomiliki maghala ya mafuta kufunga flowmeter katika mabomba yote yanayoingia kwenye maghala yao ili kuhakikisha mafuta yanapokelewa sehemu iliyokusidiwa. Serikali kupitia Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) inaendelea na utaratibu wa upatikanaji wa teknolojia (SCADA) itakayosoma flowmeter zote wakati wote ili kutambua matatizo yatakayojitokeza mapema iwezekanavyo," alisema.

Alisema Serikali kupitia PBPA imeendelea kusimamia mpangilio wa meli zinazoleta mafuta nchini ili kupunguza siku za meli kusubiri (demurrage) kushusha mafuta kutoka katika meli ambapo wastani wa siku za kusubiri kwa sasa ni siku tano (5) ikilinganishwa na wastani wa siku 75 kwa mwaka 2015.



## Maofisa ugani sasa kuvaa sare maalum

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imesema itarudisha utaratibu wa awali wa maofisa ugani kuvaa sare maalum za kuwatambulisha kama ilivyokuwa kwa mabwana shamba miaka iliyopita.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akishuhudia majaribio ya kupima aina ya udongo kwa kutumia kifaa maalum kiitwacho 'soil kit', kwenye maabara iliyopo Nzuguni jijini hapa.

Alisema serikali itahakikisha mabwana shamba wanarudi shambani, lakini wanapewa mafunzo ili kuendana na teknolojia za kisasa.

Bashe alisema wizara hiyo imejipanga kuwapa mafunzo maofisa ugani wa 1,500 na kuwapatia kifaa cha kupimia udongo ili kuwapa uhakika wakulima aina ya mazao wanayotakiwa kulima kwenye maeneo husika.

"Tunataka mabwana shamba warudi shambani, tunataka kiwe kilimo chenye tija sio cha kubahatisha, na haya mafunzo tutayatoa mara kwa mara ili kuendana na kasi ya matumizi ya teknolojia za kisasa," alisema.

Alibainisha kuwa wizara hiyo imeandaa kituo cha kilimo Bihawana kwa ajili ya kuwapa mafunzo ili waendane na teknolojia ya sasa.

"Mkakati huu wa mafunzo utaanzia katika mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Simiyu ambayo imepewa kipaumbele katika uzalishaji wa zao la alizeti," alisema.

Aidha, alisema watapewa mafunzo ya namna ya kuvitumia hivyo vifaa vya kupimia udongo ambavyo vitatoa ripoti kwa kuchapisha aina ya udongo na unafaa kulima zao gani.

"Hili tunatarajia kuanza Julai Mosi na litaendelea ili tufanikishe tija katika sekta ya kilimo na ndio lengo kuu tulilonalo kama wizara," alisema Bashe.

Kadhalika, alisema ni lazima kuwapo na uboreshaji wa upatikanaji wa pembejeo, utafiti wa maendeleo, mbegu bora na miundombinu ya mfumo wa umwagiliaji.

Alishukuru Taasisi ya Lutheran kwa kubuni teknolojia rahisi ya kusaidia wakulima kujua aina ya mazao wanayotakiwa kulima baada ya kupata majibu ya kipimo cha afya ya udongo.

Kwa mujibu wa Bashe, kila kijiji kitakuwa na shamba darasa ambalo litakuwa likisimamiwa na ofisa ugani na litagharamiwa na serikali.

Naye Mwakilishi kutoka Taasisi ya Lutheran, Moses Kabongo, alisema kifaa hicho kitasaidia wakulima kujua afya ya udongo na kuwapa tija kwenye kilimo chao.

# NARCO yaonyeshwa fursa uzalishaji malisho ya mifugo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji imeshauri Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kuanza kuzalisha malisho ya mifugo ili kusaidia wafugaji wanaozunguka ranchi hizo.

Akizungumza jana kwenye semina iliyoandaliwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia kampuni hiyo kwa ajili ya kuwajengea uelewa wajumbe kuhusu majukumu ya NARCO, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Christine Ishengoma, alisema sasa ni wakati muafaka kwa Ranchi za Taifa kuanza kuzalisha malisho.

Aidha, alishauri ranchi hizo zitumike kama mashamba darasa ambapo wafugaji hasa wa maeneo ya jirani watapata elimu juu ya ufugaji bora.

Akichangia katika semina hiyo, Mbunge wa Moshi Vijijini (CCM), Prof. Patrick Ndakidemi, alisema kamati hiyo inapaswa kuisaidia NARCO.

Alisema tayari kampuni hiyo imeshaandaa andiko mradi, ni vema wajumbe hao wakalisoma hilo andiko na kuona ni maeneo yapi kamati inaweza kuisaidia ili NARCO ipate mafanikio.

"Niwasihi NARCO kuendelea kuyatunza na kuyalinda maeneo yao kwani yanawasaidia wafugaji wenye changamoto ya maeneo ya malisho kwa kuwakodishia," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema wizara imeamua kufanya semina kuhusu NARCO ili wajumbe wa kamati hiyo wapate uelewa na kutoa maoni yao ambayo yatasaidia kuimarisha kampuni hiyo kwa kuongeza uzalishaji wa mitamba, nyama na kuzidi kuchangia kwenye pato la taifa.

Alisema kampuni hiyo ilipita katika kipindi kigumu na hivyo kushindwa kujiendesha lakini kutokana na jitihada mbalimbali zilizofanywa na wizara kwa sasa kampuni hiyo inajiendesha yenyewe.

Awali taarifa iliyowasilishwa kwa kamati, iliainisha mafanikio yaliyopatikana, mipango iliyopo ya kuongeza uzalishaji na maeneo ya vipaumbele yaliyopo katika bajeti ya mwaka 2021/2022 ikiwamo kuboresha ranchi tano za Kongwa, Ruvu, Kalambo, Missenyi na West Kilimanjaro ili kuongeza tija katika mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo.

Pia ilieleza mikakati ya kudhibiti vifo vya mifugo kwa kiwango kisichozidi asilimia mbili ya wastani wa mifugo, kuongeza na kuboresha nyanda za malisho kwa kudhibiti na kuondoa vichaka na kuimarisha vyanzo vya maji na kuweka alama za kuonekana katika mipaka ya ranchi, kuondoa wavamizi na kuimarisha ulinzi wa mipaka.



Mbunge wa Jimbo la Dodoma, Anthony Mavunde, akimkabidhi hati mmoja wa wananchi wa Mtaa wa Miganga, mkoani Dodoma, katika zoezi la kukabidhi hati kwa wananchi waliorasimishiwa makazi yao mitaa ya Miganga na Chinyika mkoani humo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Wahudumu afya wataka elimu lugha ya alama

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAHUDUMU wa afya wameiomba serikali kuwapatia mafunzo ya lugha ya alama, ili kutoa huduma ipasavyo kwa watu wenye ulemavu wa kutosikia.

Ombi hilo lilitolewa juzi jijini hapa na Dk. Sarah Mwakasege kutoka Hospitali ya Mirembe, alipokuwa akiwasilisha mada kwa washiriki wa sekta ya afya kwenye mafunzo ya lugha ya alama yaliyofadhiliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Foundation for Civil Society (FCS).

Alisema serikali ikiwapatia mafunzo hayo, yatasaidia watu hao kupata huduma stahiki kwenye vituo vya afya, zahanati na hospitali.

"Wahuduma wa afya, zahanati na hospitalini bado kuna changamoto kubwa jinsi ya kuwahudumia viziwi, kwa kuwa walio wengi hawafahamu lugha hiyo ya viziwi," alisema.

Kwa upande wake, Askofu Mkuu wa Kanisa la Bethel Baptitist Deaf Church Tanzania (BBDCT), Frenk Sarungi, alisema kukosekana kwa madawati na miongozo kwenye vituo vya afya kumechangia kwa kiasi kikubwa kuwapo na mazingira magumu ya upatikanaji wa huduma ya afya kwa watu wenye ulemavu huo.

Sarungi alisema kukosekana kwa mawasiliano kupitia miongozo na madawati ya afya ya watu wenye ulemavu wasiosikia walio wengi wamekuwa wakikosa huduma ya kiafya kulingana na mahitaji yao ya kimatibabu.

"Inasikitisha makundi ya watu wenye ulemavu mkoa wa Dodoma, walio wengi hawajui wajibu wala haki yao ya upatikanaji wa huduma za afya pale wanapoumwa au kupata ajali huwa wanatapatapa hawajui pakuanzia wala pakuishia... hii yote ni kutokana na ukoefu wa madawati na miongozo ya namna ya kupata matibabu," alisema.

Naye mshiriki wa mafunzo hayo, Mathew Saffi, alisema serikali ikitoa mafunzo ya lugha ya alama kwa wahuduma hao watu wenye ulemavu watapata huduma stahiki.

"Tunalazimika kutopata matibabu husika kutokana na wahudumu wa afya hawana utaalamu wa lugha ya alama inayoweza kuwasiliana na viziwi, kutokana na changamoto waliyonayo, kuna kila sababu watumishi mbalimbali wakiwemo wa afya kujitokeza kusoma na kujua lugha ya alama," alisema.



# Madiwani waja juu mil. 500/- za barabara

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WENYEVITI wa Halmashauri za wilaya za Chunya, Busokelo na Kyela wameiomba serikali kusitisha matumizi ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya barabara yenye thamani ya Sh. milioni 500 kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wakidai madiwani hawana taarifa za miradi hiyo.

Waliotoa kauli hiyo, wakati wa kikao cha watendaji wa serikali kilichowahusisha watumishi kutoka wilaya zote za Mkoa wa Mbeya, ambapo waliibua hoja ya kutaka fedha hizo zisitishwe, wakitaka washirikishwe mjadala uliodumu kwa zaidi ya dakika 30.

Hoja hiyo iliibuka baada ya waratibu wa TARURA kutoa taarifa ya kupokea fedha zaidi ya Sh. milioni 500 kwa mwaka 2020/2021, ambazo zimeanza kutumika kwenye miradi mbalimbali ya barabara.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara, lakini alieleza kusikitishwa kutokana na madiwani kutoshirikishwa kwenye miradi hiyo wakati hali wao ndio wenye maeneo ya miradi.

"Mimi ni mwakilishi wa madiwani, lazima nishirikishwe kwenye vikao vya maamuzi na miradi, hili la TARURA... sijaambiwa chochote, mbunge wangu anatambua haya, lakini hajaniambia," alisema Mwanginde.

Aliongeza: "Napata kigugumizi sisi madiwani ndio tunajua vikwazo vya miundombinu katika maeneo yetu, leo hii TARURA mnatueleza wabunge ndio wameelekeza zitumike kwenye miradi gani... sasa, tunaomba Mkuu wa Mkoa kuingilia kati fedha hizo zisitishwe mpaka hapo taarifa itakapoletwa kwenye vikao vya baraza la madiwani na waridhie," alisema Mwanginde.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Busokelo, Anyosisye Njobelo, alisema hawaoni sababu ya kuendelea na mjadala kwenye kikao hicho mpaka hapo watakaporidhia kwenye vikao vyao vya madiwani.

Aliilalamikia TARURA kutoshirikiana na madiwani katika kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara na kushindwa kujua barabara zenye matatizo na kuiomba serikali kuimulika taasisi hiyo.

Meya wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Dourmohamed Issa, aliomba serikali kabla ya kutoa fedha za miradi madiwani washirikishwe ili kuondoa sintofahamu, na kwamba TARURA wanapoitwa kwenye vikao kutoa maelezo hawahudhurii.

Mratibu wa TARURA Mkoa, Wilson Mwita, alisema yeye ni mgeni hivyo atahakikisha analishughulikia suala hilo na kuwahakikishia katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 madiwani watashirikishwa katika fedha za miradi zitakazotolewa.

Kutokana na malalamiko hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliagiza kusitishwa kwa kikao baina ya wabunge wa majimbo husika, TARURA, madiwani na wakurugenzi kujadili suala hilo na kuliweka sawa ili kutekeleza kwa pamoja miradi ya barabara.

"TARURA mnalalamikiwa sana kuna miradi ya barabara ambazo nimepita ni mbovu na ziko chini ya kiwango, sasa mjitathmini na msiingize siasa kwenye miradi ambayo serikali inawekeza fedha nyingi nitafanya ziara ya kukagua miradi na kujiridhisha," alisema Homera.



Wataalamu wa Jotoardhi kutoka kampuni ya TGDC kwa kushirikiana na STAMICO wakiendelea na uchorongaji visima katika eneo la Kyejo- Mbaka lilipo Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya kwa ajili ya uzalishaji wa nishati ya umeme mwishoni kwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waliopitiwa mradi wa maji kulipwa fidia

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbeya, imeitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) kuwalipa fidia wananchi wote waliopitisha mradi wa maji wa Mwashali-Isyesye ili uwe endelevu.

Aidha, imeiagiza mamlaka hiyo kuhakikisha mitaa yote inayokizunguka chanzo hicho inakuwa ya kwanza kunufaika na mradi huo ili kuimarisha ulinzi kwa kuwashirikisha wananchi hao.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alitoa agizo hilo juzi kamati hiyo ilipofanya ziara kwenye chanzo hicho kwa lengo la kuangalia hali ya ujenzi wake na kuwasikiliza wananchi watakaonufaika na mradi.

Ntinika alisema ili mradi huo uwe na manufaa kwa wananchi, ni lazima mitaa yote iliyokusudiwa kunufaika ipelekewe huduma hiyo haraka na kwamba mradi huo ni miongoni mwa miradi muhimu kwa wakazi wa Kata ya Isyesye ambao kwa muda mrefu walikuwa hawapati huduma.

"Lakini tunawaagiza mwendelee kushirikiana na wananchi wa maeneo haya kwenye ulinzi wa mradi huu, maana mlinzi wa kwanza ni mwananchi ambaye ndiye wa kwanza kunufaika na mradi husika na niwaambie tu kwamba sisi kama kamati tumeridhika na kazi ambayo mnaifanya," alisema Ntinika.

Aliwataka wananchi wa maeneo hayo kuendelea kuvitunza vyanzo vya maji ili viwanufaishe kwa muda mrefu na kwamba hawatakiwi kufanya shughuli zozote za kibinadamu kwenye maeneo hayo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mbeya-WSSA, Edina Mwaigomole, alisema wakati wa ujenzi wa mradi huo wananchi wa mitaa inayozunguka walishirikishwa katika hatua zote na kwamba wengi waliajiriwa.

Alisema eneo ambalo wamejenga mradi huo ni lenye mwinuko mkali ambao hauruhusu magari kufika na hivyo waliamua kuwaajiri wananchi kubeba vifaa na kuvipandisha mpaka kwenye eneo la ujenzi.

Alisema kutokana na hali hiyo wana uhakika kwamba wananchi hao wataendelea kushirikiana na mamlaka kulinda miundombinu ya mradi huo hata baada ya kukamilika na kuanza kutumika.

"Walifurahi kwanza kwa kuajiriwa na sisi, hili eneo lilikuwa haliwezekani kabisa kufikisha vifaa, sasa tuliamua kuwashirikisha wenyekiti kufanya kazi hii na ndio maana mnaona mradi umefikia hatua hii," alisema Mwaigomole.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Kaimu Mkurugenzi wa Mradi huo, Mhandisi Barnabas Konga, alisema miradi yote ambayo mamlaka hiyo imekuwa ikitekeleza inawatumia wataalamu wa ndani badala ya kuwatumia makandarasi ili kupunguza gharama.

Alisema mfumo huo wa utekelezaji wa miradi unaokoa zaidi ya asilimia 50 ya gharama za utekelezaji kwa maelezo kuwa baadhi ya miradi ikijengwa na mkandarasi huwa wanalazimika kuajiri na mkandarasi mshauri, hatua ambayo huongeza gharama.

Alisema kwenye ulinzi wa vyanzo vya maji wamekuwa wakitumia makampuni binafsi ya ulinzi, kamera za ulinzi (CCTV) na kuzungushia uzio kwenye kila mradi.

# Maelfu ya vijana wachangamkia masomo VETA

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIJANA 6,900 kati ya 8,995 kutoka maeneo mbalimbali nchini, wamerejesha fomu kwa ajili ya kuanza katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), Nyanda za Juu Kusini mkoani Mbeya.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi VETA, Mhandisi Hassan Kalima, alisema idadi ya vijana walijitokeza ni kubwa na walionyesha nia ya kuhitaji kupata elimu kama nyenzo ya kujiajiri na kujikwamua kiuchumi.

Alisema mahitaji ya vijana kupata elimu ya ufundi stadi ni makubwa kutokana na idadi ya waliochukua fomu pekee ni 8,995, huku waliorejesha ni 6,900.

"VETA Mbeya tulipokea maombi 8,995 kwa ajili ya mafunzo yaliyofadhiliwa na serikali, lakini waliorejesha fomu walikuwa ni 6,900, tumeshakamilisha mchakato, lakini kwa taarifa nilizopata ni kwamba vijana wote walioomba watafikiwa na wataendelea kupata mafunzo stadi ya ufundi," alisema Kalima.

Mhandisi Kalima alisema idadi ya wanafunzi wanaopeleka maombi ni kubwa na kwamba ili kukidhi mahitaji, serikali inaboresha mabweni na karakana katika chuo hicho pamoja na ujenzi wa vyuo vya VETA katika wilaya za Ileje na Mbarali.

Alisema kwa mwaka 2021, jumla ya wanafunzi 159 walihitimu mafunzo ya ufundi katika fani mbalimbali ngazi ya tatu ambayo yalitolewa kwa miaka mitatu.

Alisema kati yao wanaume ni 140 na wanawake ni 19 na kwamba fani ni za uashi, uchomeleaji, ufundi magari, umeme wa majumbani na wa magari.

Mwakilishi wa Jeshi la Polisi Dawati la Jinsia, Immaculate Mwalanda, alisema ni wakati sasa vijana kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali kuwa chachu ya kupata ujuzi na kujiajiri katika nyanja mbalimbali za ufundi ili kujiingizia kipato na kukitangaza chuo cha VETA ndani na nje ya nchi.



# Mtuhumiwa ubakaji anusurika kuuawa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limelazimika kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya wananchi waliokuwa na hasira waliotaka kumshambulia kijana anayedaiwa kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka 10.

Pamoja tuhuma za ubakaji mtuhumiwa huyo katika siku hiyo hiyo moja anadaiwa kujaribu kumbaka mtoto mwingine mwenye umri wa miaka 14 na kumpora mwanamke mkoba wenye fedha.

Katika tukio hilo la tuhuma za ubakaji ambalo lilitokea juzi majira ya saa tatu asubuhi, mtuhumiwa huyo alilazimika kuhifadhiwa katika nyumba ya Sheha wa Shehia ya Kisauni nje kidogo na Mji wa Zanzibar, ili wananchi wenye hasira wasimdhuru.

Awali, wananchi waliokuwa na hasira walitaka kumpiga na kutishia kumuua baada ya kushuhudiwa akimfanyia kitendo cha ubakaji mtoto huyo.

Nipashe ilishuhudia kundi kubwa la watu wakiwa nje ya nyumba ya Sheha wa Shehia hiyo huku taratibu za kumkinga na kumhami mtuhumiwa huyo ili asidhuriwe na watu hao zikifanyika, lakini akiwa ameshachezea kipigo cha wananchi hao.

"Wananchi walikuwa na hasira sana kutokana na vitendo hivi ambavyo vinatokea kila siku na kuendelea kuwadhalilisha watoto na ndio maana wananchi wamechoshwa, na kama si Jeshi la Polisi yule kijana angeuliwa kabisa kutokana na hasira za watu," alisema Khamis Ali, shuhuda aliyekuwa nje ya nyumba ya sheha.

Wananchi hao wameviomba vyombo vya sheria kuhakikisha wanatoa adhabu kali kwa mujibu wa sheria kwa watuhumiwa wa vitendo vya udhalilishaji, pamoja na kuwadhibiti wasitoroke na kutumikia adhabu zao wanazohukumiwa.

Awali, wananchi hao walikusanyika nje ya nyumba ya sheha wakitaka mtuhumiwa huyo atolewe wampige huku wakijaribu kuvunja milango, lakini sheha alikuwa ameshatoa taarifa polisi ili mtuhumiwa achukuliwe na kupelekwa katika vyombo vya sheria.

Askari wachache walifika katika tukio hilo, lakini walizidiwa nguvu na wananchi waliokuwa na hasira na kulazimika kuongeza nguvu kwa kuita askari wengine na kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya wananchi hao katika eneo hilo.

Sheha wa Kisauni, Hija Suleiman, alisema mtuhumiwa huyo alifikishwa kwake baada ya kukutwa akimfanyia kitendo cha udhalilishaji mtoto huyo mwanafunzi wa shule ya msingi.




"Wananchi walikuwa na hasira sana kama nisingemfungia ndani mwangu wangemuua," alisema.

Sheha Suleiman alisema mtoto huyo aliyefanyiwa udhalilishaji ni mkazi wa shehia yake, lakini mtuhumiwa hakai kwenye shehia hiyo.

Shuhuda wa tukio hilo, Mundhir Ali Bakar, alisema alimkuta mtuhumiwa katika jumba bovu eneo la Kisauni Kidutani akimfanyia mtoto kitendo hicho na alipoona kuwa ameshafumwa alikimbia.

Alisema alipambana naye kumfukuza na hatimaye alimkamata na kuomba msaada kwa watu wengine ambao walifika katika eneo hilo kuja kumsaidia.

"Wakati napita eneo la tukio nilimsikia mtoto analia anapiga kelele sana sauti iliyoashiria anafanyiwa kitu kibaya katika jumba bovu na nilipoangalia nikamkuta tayari ameshamvua nguo anamfanyia kitendo cha udhalilishaji huku akiwa amemwekea kisu shingoni," alisema shuhuda huyo.

Aidha, alisema wakati anapambana na mtuhumiwa huyo alitoa kisu na kumpiga nacho mkononi, lakini wakifanikiwa kumkamata na kumpeleka kwa sheha kwa hatua nyingine zaidi.

Akielezea kilichomtokea mtoto huyo alisema, alitoka kwao kuelekea madrasa na alipokuwa njiani alitokea mtu huyo akiwa amepanda bodaboda na kumwambia apande katika bodaboda amuwahishe ili asichelewe.

"Kasimamisha bodaboda yake akaniambia panda nikupeleke, nikapanda, nilipofika eneo la madrasa nilimwambia kuwa nimeshafika, lakini alikataa kunishusha nikaanza kupiga kelele, lakini alipeleka mbio bodaboda na kunipeleka katika lile jumba na kuniambia nikipiga kelele ataniua," alisema mtoto huyo huku akilia.

Mtuhumiwa wa tukio hilo, Idrisa Juma Pandu, alikiri kufanya tukio hilo na kusema kuwa haikuwa akili yake kwa kudai alikuwa anafanya jambo hilo bila ya kutarajia.

Akizungumzia tukio hilo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Awadhi Juma (pichani), alisema kuwa mtuhumiwa huyo yupo Kituo cha Polisi Mazizini kwa hatua za kisheria.

Alisema mtuhumiwa huyo anakabiliwa na malalamiko matatu ambayo yameripotiwa kituoni hapo, yaliibuka baada ya wananchi kusikia amekamatwa mtu kwa kosa la ubakaji na ndipo wengine wakaenda kushuhudia mtu huyo na kumbaini kuwa ni yeye.

Kamanda Awadh aliwaambia waandishi wa habari kwamba matukio yote hayo ya uhalifu ameyafanya kijana huyo kwa siku moja kwa nyakati tofauti na maeneo tofauti.

Alisema kabla ya kufanya ubakaji, majira ya saa 12 asubuhi kijana huyo alimpora mama mmoja mkoba wake ukiwa na simu na fedha, baadaye majira ya saa moja asubuhi alitaka kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka 14 eneo la Mombasa Mbuyumnene, lakini mtoto huyo alifanikiwa kukimbia.

"Huyu kijana anaonesha amekusudia kweli kwa sababu kuna mtoto hapa amempakia halafu yule mtoto akapiga kelele na akachupa kwenye bodaboda yake, inaonyesha alikuwa anataka kutenda kitendo kiovu maana huyu mtoto anasema kila akimwambia nishushe ndiyo anazidisha mwendo, lakini Mungu akamjaalia akachupa akaanguka chini na kukimbilia kwao," alisema jirani mmoja wa Mombasa.

Alisema baada ya kumkosa mtoto huyo ndipo alipokwenda kumdhalilisha mtoto wa miaka 10 eneo la Kisauni na kuonekana na kijana mmoja ambaye alipambana naye na kisha kufanikiwa kuwaita watu waje kumsaidia kabla ya kupelekwa kwa Sheha.

Kamanda Awadh alikiri kuwa Jeshi la Polisi lililazimika kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya wananchi waliokuwa na hasira kutaka kumshambulia mtuhumiwa huyo ili wasimdhuru.

Alisema ni kweli vitendo hivyo vinaumiza, lakini amewataka wananchi kutochukua sheria mikononi kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria na huenda wakajikuta nao wanafanya makosa makubwa.

Mweka hazina mkuu wa jumuiya ya bodaboda, Mohammed Mahmoud Hassan, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kwa wanaotaka kupanda bodaboda kuhakikisha wanachukua namba ya simu, na kuchukua namba za vikoti wanavyovaa ili inapotokea jambo lolote waweze kuripoti namba hizo ili watafutwe.

"Nawashauri wanaotaka kupanda bodaboda wachukue tahadhari namba za simu na namba ya kikoti anachovaa dereva wa bodaboda kwa sababu unapochukua namba yake anapofanya jambo lolote la kihalifu atapatikana kwa kutokana na namba hizo, ni muhimu sana," alisema Hassan.

Aliliomba Jeshi la Polisi kuwachukuliwe hatua za kisheria ili iwe funzo kwa wengine wenye tabia kama hizo za udhalilishaji.

Wakati hayo yakijiri Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar), Dk. Mzuri Issa, amewashauri wazazi na walezi kuhakikisha wanafuatilia vyema nyendo za watoto wao wakati wanapokuwa nje ya nyumba zao ili kuepukana na vitendo vya udhalilishaji.

Dk. Mzuri alisema suala la ulezi wa watoto ni kila mahali ikiwamo maeneo wanayocheza, wanayosoma na yalio nje ya nyumba zao.

## SMZ kuendelea kusimamia uendeshwaji msaada kisheria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kusimamia uendeshwaji wa msaada wa kisheria ili kufikia maendeleo ya kiuchumi.

Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud, aliyasema hayo wakati akizungumza katika maadhimisho ya pili ya wiki ya msaada wa kisheria yaliyofanyika mjini Unguja.

Othman alisema suala la msaada wa kisheria sio la huduma pekee za kisheria bali kimataifa na limekubalika na kutambulika kuwa ni nyenzo muhimu ya kuleta maendeleo katika taifa na kupunguza umaskini.

"Kuanzisha mfumo rasmi wa msaada wa kisheria nchini ni sehemu ya juhudi ya serikali kutambua kuwa Zanzibar inahitaji kuweka mifumo inayoendana na maendeleo ya kidunia katika fani na nyanja zote," alisema.

Alisema mbali na umoja wa mataifa umuhimu wa msaada wa kisheria umetambuliwa pia na maazimio mbalimbali ya nchi za Afrika kwa lengo la kutilia mkazo suala la msaada wa kisheria katika nyanja mbalimbali.

"Sheria ya msaada wa kisheria namba 13 ya mwaka 2018 pamoja na kanuni zake za mwaka 2019 ni mkombozi mkubwa kwa watu wasiokuwa na uwezo wakiwamo wanawake na watoto," alisema.

Alitaka idara ya msaada wa kisheria kupitia vizuri miongozo hiyo kwa lengo la kuona msaada wa kisheria unapatikana bila ya matatizo.

Kwa upande mwingine Makamu wa Kwanza huyo, aliwahimiza watoa huduma za msaada wa kisheria kuzingatia haki za makundi mbalimbali ya binadamu pamoja na matatizo yaliyomo katika jamii ikiwamo migogoro ya ardhi na unyanyasaji wa kijinsia ili iwe ni kiashiria kikuu cha kupatikana kwa haki katika jamii ya Zanzibar.

Amezipongeza taasisi za serikali na zisizo za serikali kwa juhudi wanazozichukua katika kuwafikia wananchi na kuwafahamisha upatikanaji wa msaada wa kisheria.

Akitoa maelezo mafupi kuhusu maadhimisho hayo, Mkurugenzi wa Idara ya Msaada kisheria, Hanifa Ramadhan Said, alisema idara imejipanga kuanzisha wasaidizi wa kisheria katika kila wilaya kwa lengo la kuona upatikanaji wa msaada wa kisheria unakuwa mwepesi ili wananchi wapate haki zao.

Alisema lengo la kaulimbiu ya mwaka huu ni kuona mwanamke anakomboka kiuchumi na kupata sehemu ya kumuwezesha kisheria pamoja na kuona huduma za kisheria zinatolewa maeneo mbalimbali.

Meneja Mkuu wa mradi wa shirika la msaada wa kisheria Tanzania (LSF), Deogratias Bwire, aliahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Idara ya msaada wa kisheria ili kuendeleza kazi za wasaidizi wa kisheria kwa lengo la kuwanufaisha wananchi kutokana na matatizo yanoyohusu sheria.

## Balozi EU afurahia mradi wa viungo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BALOZI wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania, Manfredo Fanti, ameeleza kufurahishwa na utekelezaji wa mradi wa viungo visiwani Zanzibar na kuwa ana matumaini kuwa mradi wa kilimo cha mboga, matunda na viungo utapunguza na kuondoa umaskini kwa wakulima wengi.

Aliyasema hayo wakati wa ziara maalumu ya kutembelea baadhi ya mashamba ya wakulima katika shehia ya kizimbani na Biguni, Unguja.

Alisema kilimo hicho ni miongoni mwa sekta muhimu ambayo ikitumiwa vyema itabadilisha maisha ya wakulima na kuzalisha kwa wingi, mazao yenye ubora na kupata soko la uhakika.

Aliwata wakulima hao kutokata tamaa, waendelee kuitumia fursa zinazopatikana kupitia mradi huo.

Alisema ushiriki mkubwa na utayari wa kujifunza walioouonesha wakulima wengi unatia moyo na anaamini kwamba elimu waliyoipata wataitumia vyema kuendeleza kilimo chao kwa manufaa yao jamii na taifa kwa ujumla.

Aliwataka wanufaika wa mradi kuitumia fursa hiyo kama sehemu muhimu ya kujifunza na kuongeza uelewa kupitia aina mbalimbali mpya za kilimo ambazo hazikuwa zikitumiwa awali.

Baadhi ya wanufaika wa mradi huo, Haji Abdallah Abeid, ambaye ni mkulima wa vanila, alisema elimu aliyoipata kupitia mradi wa viungo imemsaidia kuimarisha kilimo chake na ameanza kuona mabadiliko makubwa jinsi ya ulimaji wake kuanzia utayarishaji wa shamba, upandaji na anaamini atavuna mazao mengi na bora.

"Nimefanya shughuli za kilimo hiki kwa miaka mingi, lakini kwa njia za kienyeji ambazo hazikuniwezesha kupata mafanikio ninayoyatarajia, lakini sasa kupitia elimu hii na utaalamu tunaoupata kutoka mradi wa viungo ninaamini ndoto yangu itatimia," alisema Haji.

Alisema kupitia mradi huo wa viungo amejifunza njia mpya za kilimo hicho cha vanila na tayari ameanza kuzifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuanzisha shamba jingine jipya ambalo tayari ameotesha miche zaidi ya 200.

Alisema kuwa kupitia mashamba darasa yanayoanzishwa kila shehia na mradi wa viungo yatasaidia kwa kiasi kikubwa kuendelea kujifunza mbinu mbalimbali ambazo zitaleta mafanikio makubwa kwa wakulima wa mboga, matunda na viungo ambao ndio wanufaika wa mradi huo.

Akizungumzia hali ya soko la vanila, alisema kwa sasa kilo moja ya vanila wanauza kwa Sh. milioni 1.6 na kupitia mradi huo anaimani soko la bidhaa hiyo litakua zaidi na wataongeza uzalishaji na ubora wa vanila.

Kwa upande wake mkulima wa matunda Shehia ya Binguni, Namri Najim, alisema mfumo mpya wa kilimo unaozingatia elimu, utaleta tija kwao na kuzalisha bidhaa nyingi zaidi.

# Waomba vifurushi vya NHIF vijumuishe wenye selimundu

**Na Elizabeth Zaya**

JAMII ya watu wanaoishi na ugonjwa wa selimundu wameiomba Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuweka mpango utakaowezesha dawa zote za ugonjwa huo kujumuishwa katika vifurushi vyote vya Mpango wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ili kuwarahisishia upatikanaji wa matibabu kwa haraka.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Wagonjwa wa Selimundu Tanzania, Arafa Said, alisema bado kuna baadhi ya hospitali hazijajumuisha baadhi ya dawa ugonjwa wa selimundu katika bima ya afya na huwalazimu wagonjwa wa ugonjwa huo kutumia gharama kubwa kuzinunua na wengine kushindwa kumudu gharama zake.

"Tunafahamu kwamba kuna dawa za selimundu zilijumuishwa kwenye bima ya afya, lakini bado baadhi ya hospitali nchini tumekuwa tukipata malalamiko kwamba wagonjwa hawa wanapokwenda katika hospitali hizo kutafuta huduma za matibabu hawapatiwi baadhi ya dawa kwa madai kwamba hazijajumuishwa katika bima, hili ni tatizo kubwa," alisema Arafa.

Alitaja miongoni mwa dawa ambazo utolewaji wake umekuwa changamoto katika hospitali nyingi kuwa ni pamoja na Hydroxyurea.

Pia aliiomba serikali kuweka sera na mipango ambayo itaboresha utoaji wa huduma za afya kwa kundi hilo na upatikanaji wa huduma za kliniki za selimundu katika kila mkoa.

"Bado hakuna vituo vya afya au kliniki za kutosha za kutoa huduma au vipimo kwa wagonjwa wa selimundu, wagonjwa wengi hulazimika kusafiri mpaka Dar es Salaam kufuata huduma, hili nalo ni tatizo kubwa, tunahitaji kliniki na huduma kwa wagonjwa hawa zipanuliwe wigo mpaka vijijini huko katika kila mkoa ili wasipate changamoto ya kukosa matibabu, tunaiomba serikali iliangalie kwa uzito wa kipekee," alisema Arafa.

"Bado kundi hili linahitaji matibabu ya haraka pale wanapoyahitaji pamoja na wauguzi ambao wana elimu na uelewa mzuri juu ya selimundu, tunahitaji maabara zenye ubora zitakazotoa vipimo na majibu ya uhakika."

Miongoni mwa wanaougua ugonjwa huo, Othman Shaban, alisema kwa sasa upatikanaji wa huduma na dawa si wa kuridhisha na kwamba wanalazimika kutumia gharama kubwa kununua dawa hizo.

"Kwa kweli bado tunaendelea kuisisitiza serikali itusaidie katika hili la kuboresha huduma za kliniki na dawa, kwanza ukitaka kwenda kliniki lazime usafiri kwenda Dar es Salaam, lakini ukifika bado kuna baadhi ya dawa haupatiwi, unaambiwa ukanunue na boksi moja tunanunua kuanzia Sh. 40,000 hadi Sh. 60,000, hii ni changamoto kubwa sana kwetu, tunaomba serikali itusaidie," alisema Shaban.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Jenista Mhagama (katikati) akijadiliana jambo na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma ( kulia), Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Najma Giga na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Profesa Jamal Adam, wakati wa ziara ya Kamati hiyo kutembelea Ofisi za Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye mimba shuleni walivyopungua Muleba

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

IDADI ya wanafunzi waliopata mimba wakiwa shuleni katika wilaya ya Muleba mkoani Kagera, imepungua kutoka zaidi ya 100 mwaka 2017 hadi kufikia 15 mwaka 2020.

Akizungumza na Nipashe kwa niaba ya afisa elimu sekondari wa wilaya hiyo, Afisa Elimu (Taaluma), Godelva Ngirwa, alisema idadi hiyo imepungua kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuundwa kwa kamati ya kudhibiti mimba na utoro shuleni.

Aidha, Ngirwa alisema kwamba katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Aprili mwaka huu, wanafunzi waliobainika kupata mimba ni wanne tu tofauti na zamani, ambapo wanafunzi waliokuwa wakipata mimba katika kipindi kama hicho walikuwa kati ya 15 hadi 20.

"Tumetoa sana elimu na tunaendelea kufanya hivyo hadi vitendo hivi vitakapokwisha kabisa katika wilaya yetu," alisema.

Alisema kamati hiyo imekuwa ikifuatilia wanafunzi kwa ukaribu zaidi shuleni, kutoa elimu kwa wanafunzi na walimu (hasa kwa walimu wanaohusika na malezi) na kuwachukulia hatua wote wanaobainika kuhusika na mimba za wanafunzi.

"Kama kuna mtoto kapewa mimba na ikabainika kuna mambo yanafichwa, kamati imekuwa ikinyanyuka na kwenda kufuatilia na kuhakikisha kama kuna mtuhumiwa hajakamatwa basi atafutwe na akipatikana achukuliwe hatua za kisheria," alisema.

Alitaja baadhi ya sababu zinazochangia mimba shuleni ni malezi duni ya wazazi kwa watoto wao, watoto kukosa matumizi kutoka kwa wazazi na kusababisha waanze kutafuta wanachokihitaji na watoto kutojitambua, wakikutana na watu wa kuwadanganya ni rahisi kudanganyika.

Naye mwenyekiti wa kamati ya elimu, afya na maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Evath Tilwetwa, alisema mimba shuleni zipo na ndiyo maana wanapata kesi nyingi zinazohusiana na wanafunzi kubeba mimba.

Mmoja wa wanafuanzi walipata mimba wakiwa shuleni Olvia Anselimi (19), mkazi wa Magata wilayani Muleba, alisema migogoro ya familia imechangia kupata ujauzito na kufukuzwa shule mwaka huu akiwa kidato cha nne, katika shule ya sekondari Kishoju iliyoko wilayani humo. Olvia ambaye anatarajia kujifungua mwezi Septemba 2021, alisema sasa ana muda wa miezi takriban minne tangu amefukuzwa shule, lakini anashukuru Mungu wazazi hawajamfukuza nyumbani ingawa anapitia mateso ya kutegemea matumizi kutoka kwa mama yake mzazi asiye na kipato cha uhakika.

Alisema kilichosababisha kupata mimba ni migogoro ya kifamilia kati ya mama yake mzazi na baba yake ambayo iliwafanya wazazi wake hao kukosa muda wa kumsikiliza na kutatua changamoto zilizokuwa zikimkabili, hali iliyomfanya kukata tamaa na kutafuta faraja kwingine.

Mkurugenzi mtendaji wa mtandao wa mashirika yanayotoa msaada wa kisheria, Christina Ruhinda, alisema ili kupunguza vitendo vya mimba shuleni, wameanzisha klabu shuleni ambazo zinazungumzia ukatili wa kijinsia, upatikanaji haki na huduma za kisheria.

HABARI KITAIFA

# Profesa ataka wakufunzi mijadala elimu yenye tija

Na Mwandishi Wetu, MASASI

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo, ametoa wito kwa wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC) kufanya mijadala ya pamoja ya namna ya kuboresha elimu ya ujuzi inayotolewa katika vyuo hivyo.

Alitoa rai hiyo wakati akikagua kazi ya uboreshaji wa miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Masasi.

Prof. Nombo alisema hivi sasa kuna mijadala mingi inayoendelea kuhusu utoaji wa elimu ya ujuzi na maarifa kwa vijana, hivyo ni vyema wakufunzi wakafanya tathmini ya pamoja juu ya namna nzuri ya kutoa elimu hiyo, kwa kuzingatia mahitaji ya soko.

Alisema ili kuwezesha vijana kuweza kuajiriwa na kijiajiri bila changamoto yoyote ni muhimu ujuzi wanaopatiwa uboreshwe mara kwa mara, ili kuwezesha kuendana na mabadiliko ya wakati, soko na teknolojia.

Prof. Nombo alisema katika kufikia malengo hayo wakufunzi wanahitaji kufanya jitihada za kuboresha upatikanaji wa ujuzi.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Seleman Mzee, aliishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa namna inavyotekeleza miradi mbalimbali ya kuboresha elimu Wilaya Masasi.

Alisema mafunzo yanayotolewa katika chuo hicho yamewezesha vijana wengi kutoka Wilaya ya Masasi kuajiriwa huku wengi wakiwa wamejiajiri.

Mkuu wa Chuo cha Wananchi Masasi, Sophia Mkope alisema chuo hicho kina wanafunzi 400 na kinatoa mafunzo katika fani mbalimbali ambazo zimekuwa zikiwasaidia vijana kupata ujuzi na maarifa.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akikagua bei ya zao la pamba jana, katika ziara yake ya kukagua maendeleo ya masoko ya pamba na kuhamasisha wakulima wa zao hilo kulima kwa wingi alizeti, choroko, dengu na pamba wilayani Igunga. **PICHA: VINCENT TIGANYA**

# Mgodi wachimba kisasa bila wafanyakazi

Na Shaban Njia, KAHAMA

MGODI wa uchimbaji madini ya dhahabu wa Barrick Bulyanhulu, ulioko Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, umetangaza kuanzisha teknolojia ya uchimbaji pasipo watu kuendesha mitambo, ili kwenda kisasa na teknolojia.

Msimamizi wa ufundi wa mgodi huo, Edwini Bushasha, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa ya mgodi kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga,Dk. Philemon Sengati, aliyefanya ziara katika mgodi huo.

"Mkuu wa Mkoa, teknolojia tunayotaka kuianzisha hivi karibuni, watumishi wanaofanya kazi chini ya ardhi, wakitoka kazini majira ya saa 11 jioni, mashine hizo zitaendelea kufanyakazi zenyewe, hivyo kuharakisha uzalishaji wa madini," alisema Bushasha.

Bushasha aliongeza kuwa: "Mitambo ya kufanyakazi bila watumishi, kwa migodi mingine ya nje ndiyo wanatumia na kwa kufanya hivi sisi tutakuwa wa kwanza kuitumia na itasaidia kuleta ufanisi wa kazi hasa chini ya ardhi."

Meneja Rasilimali watu wa Kampuni ya Barrick, Shukuru Mwainunu, alisema hadi kufikia Mei mwaka huu mgodi ulikuwa na wafanyakazi 768, huku Watanzania wakiwa ni asilimia 94.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, aliushukuru uongozi wa mgodi huo chini ya Kampuni ya Twiga kwa kuona umuhimu wa kuanzisha teknolojia ya uchimbaji wa madini kisasa na kuwataka wafanyakazi wa mgodi huo kufanyakazi kwa weledi na kufuata sheria.

Alisema kwa sasa ni lazima uchimbaji uwe wa kisasa ili kukuza uchumi na kwenda sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani.

Alisema hali hiyo itasaidia pia kuondokana na uharibifu wa mazingira mahala pakazi.

Aidha Sengati alidai kuwa endapo teknolojia hiyo itakwenda vizuri katika ufanyaji kazi mgodini, hata mapato ya halmashauri na maduhuri ya serikali yataongezeka, kwamba serikali inaendelea kusisitiza nidhami na ubunifu katika masuala mbalimbali ikiwamo uchimbaji wa madini.

Mbali na hilo, aliwapongeza kwa kuwapatia kipaumbele ajira wananchi wanaozunguka mgodi huo.

# Dawa 'fasta' malaria yazinduliwa

Na Joctan Ngelly, GEITA

KAMPUNI ya Anjata Pharmacy imezindua dawa iitwayo Artefan inayotibu ugonjwa wa malaria kwa haraka hususani kwa watoto wadogo na kwa watu wazima.

Akizungumza na madaktari, wafamasia, manesi pamoja na wadau wa afya mkoani Geita, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo, Kumar Banguru alisema dawa hiyo inatibu ugonjwa wa malaria kwa haraka tofauti na dawa zinginezo.

Banguru alisema tatizo la ugonjwa wa malaria lipo kubwa sana japo kuna juhudi mbalimbali zimefanywa na serikali na wadau mbali mbali wa afya na katika kupunguza.

"Ndiyo maana tumewaita ili tuwape taarifa kuhusu dawa hii mpya ambayo inaitwa Artefan ambapo tumetoka kwenye vidonge 24 na kwenda vidonge sita vya Aluu, ambapo watu wengi walikuwa wanashindwa kumaliza dozi lakini kwa dawa hii mpya kila mtu atakuwa anamaliza dozi kwa wakati," alisema Banguru.

Alisema programu hiyo ni endelevu katika mikoa mbalimbali hapa nchini ili kuweza kupambana na ugonjwa wa malaria ambao umeuwa watu wengi hasa watoto chini ya miaka mitano katika kipindi cha nyuma.

Aidha, aliwataka wakazi wa Mkoa wa Geita kupambana na ugonjwa wa malaria katika ngazi zote kwa kutumia vyandaluwa, kufukia madimbwi pamoja na mazingira kuwa safi.

"Lengo letu kubwa la kufanya Semina hii ni kumpa uwezo daktari na mfamasia ili kupambana na malaria kwa kusaidia jamii katika ugonjwa huu, pia kumsaidia mwananchi kuwa na afya njema kuhakikisha ugonjwa huu unatokomea, tunaungana pamoja na serikali pamoja na wadau wa afya," alisema Banguru.

Alisema Kampuni ya Anjata Pharmacy makao yake makuu yapo Mombai India, hapa nchini ina matawi katika mikoa ya Dar es salaam, Mwanza na Arusha.

Alisema pia wana dawa mpya ya kuongeza nguvu za kiume ambayo kidonge kimoja kinauzwa kwa Sh, 4,000, pamoja na dawa ya kutibu ugonjwa moyo.

# LEVY AONYA KUHUSU UVUMI WA KANE




**LONDON,** England

MWENYEKITI wa Tottenham, Daniel Levy, hajafanya chochote kushusha presha kuhusu uvumi wa majaliwa ya Harry Kane, akielezea sababu ni kutokana na matatizo ya kifedha ya Spurs, lakini amesisitiza bado wanapambana kumbakisha.

Kane amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka hapo Tottenham huku uvumi ukimhusisha na mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City pamoja na Manchester United, Chelsea, Real Madrid na Barcelona.

Levy alizungumza kupitia tovuti rasmi ya Tottenham baada ya kumteua Mkurugenzi wa Michezo wa zamani wa Juventus, Fabio Paratici kama Mkurugenzi Mkuu, akionya kuwa klabu hiyo ya London itafanya jambo lililo sahihi kwao.

"Kamwe sitazungumza kuhusu mchezaji mmoja hadharani," alisema Levy huku Tottenham ikiwa bado haina kocha mkuu baada ya kutimuliwa kwa Jose Mourinho, Aprili mwaka huu.

"Naweza kusema kwamba mkanganyiko wa kutokushinda si wake binafsi tu, kwani ni wa mimi, mashabiki pamoja na wachezaji. Wote tunataka kushinda."

Wakati huo huo, Levy amesema klabu ina matatizo makubwa ya kifedha lazima wawe "wakweli" kuhusu hali hiyo hasa ikizingatia athari walizozipata kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

"Kazi yetu ni kulinda klabu hata kama tunataka kushinda," alisema Levy. "Tutaingia sokoni, lakini tutakuwa makini sana kwa sababu ya hali yetu."

# Tite afunguka mgomo Brazil Copa America




**BRASILIA,** Brazil

KOCHA Mkuu wa Brazil, Tite amebainisha kwamba, timu hiyo haikutaka michuano ya Copa America kufanyika kwenye ardhi yao kutokana na utata uliojitokeza, lakini imewalazimu tu kucheza.

Brazil ambao ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo ya Mataifa ya Amerika Kusini, jana Jumapili walifungua dimba na Venezuela ambayo inakabiliwa na idadi kubwa ya ongezeko la virusi vya corona.

Awali, 'Selecao' hao walitaka kugomea mashindano hayo kutokana na janga hilo la corona, lakini baadaye wakaamua kuendelea nayo.

Michuano hiyo iliahirishwa mwaka 2020 kwa sababu ya mlipuko huo wa COVID-19, ambapo awali ilikuwa iandaliwe kwa ushirikiano wa nchi mbili za Colombia na Argentina, lakini baadaye nchi hizo zikaondolewa.

Brazil walipewa haki ya kuandaa michuano hiyo, licha ya nchi hiyo nayo kuwa na idadi kubwa ya maambuziki ya COVID-19.

Nahodha wa Brazil, Casemiro na kikosi hicho tayari walilishutumu Shirikisho la Soka la Amerika Kusini 9 (CONMEBOL), kwa kusema kuwa hawakuangalia ubinadamu.

# *PSG yamfungia kazi Hakimi*

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain imebakia kuwa pekee inayoongoza kwenye mbio za kumwania nyota wa Inter Milan, Achraf Hakimi, kwa mujibu wa Gianluca Di Marzio.

Hakimi amekuwa mchezaji anayewinda zaidi baada ya kuwa na msimu wake wa kwanza wa kuvutia kule Inter.

Ameisaidia Inter kutwaa taji lake la kwanza la Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 10, lakini majaliwa yake yanaonekana kuwa nje ya pale kwenye dimba la San Siro.

Na sasa PSG imeripotiwa kuingiza miguu yake yote miwili kuwania saini ya mlinzi huyo wa pembeni na kutaka kuzipiku Chelsea na Bayern Munich ambazo nazo zinawania saini yake.

PSG imetoa ofa ya Euro milioni 60 kwa mabingwa hao wa Serie A, ambao wanakabiliwa na matatizo ya kifedha yaliyosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona, huku pia kukiwa na shaka juu ya majaliwa ya nyota kama Romelu Lukaku, Lautaro Martinez na Alessandro Bastoni.

Miamba hao wa Ligue 1 sasa wanaonekana kuongoza kwenye mbio za kuinasa saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco.



## HABARI MICHEZO



# HALI YA ERIKSEN YATENGEMAA

**COPENHAGEN, Denmark**

HALI ya Christian Eriksen imetengemaa baada ya kuanguka na kuzimia uwanjani kisha kukimbizwa hospitali juzi Jumamosi jioni, limesema Shirikisho la Soka la Ulaya, Uefa.

Chama cha Soka cha Denmark, kilisema kiungo huyo wa Inter Milan, Eriksen "alizinduka" na kufanyiwa "uchunguzi wa kina wa matibabu" baada ya kudondoka uwanjani katika kipindi cha kwanza wakati nchi yake ikicheza mchezo wa ufunguzi wa michuano ya Euro 2020 dhidi ya Finland jijini Copenhagen.

Wachezaji wenzake na mwamuzi, Anthony Taylor waliwaita haraka madaktari, huku wachezaji wakimzunguka kuweka wigo wa kutopigwa picha wakati wakiwa kwenye harakati za kuokoa maisha ya Eriksen.

Uefa haraka ikasimamisha mchezo huo, lakini baadaye wachezaji wa timu zote mbili walikubaliana kuumalizia, baada tu ya kupata maendeleo ya afya ya Eriksen.

Na sasa taarifa zaidi zinasema kwamba, hali ya Eriksen imeimarika na anaendelea na matibabu na taarifa zaidi zitatolewa baadaye. Katika mchezo huo Finland iliibuka na ushindi wa bao 1-0.

## BALE: TUNAJIPANGA KWA MCHEZO WETU WA PILI

**BAKU, Azerbaijan**

GARETH Bale ana matumaini Wales watapambana sana baada ya kutoka sare ya kufungana bao 1-1 na Uswisi kwenye mchezo wao wa ufunguzi wa michuano ya Euro 2020.

Kieffer Moore alifunga bao kwa kichwa zikiwa zimesalia dakika 16 mchezo kumalizika akisawazisha lile la Breel Embolo kwenye mchezo huo wa Kundi A uliopigwa katika dimba la Baku Olympic hapa Azerbaijan.

Uswisi walifunga bao la pili kupitia kwa Mario Gavranovic, lakini VAR ilikataa kwa kuonyesha mfungaji aliotea kabla ya Moore kusawazisha na kuwafanya wagawane pointi moja moja.

Wales sasa imepoteza mchezo mmoja tu kati ya 14 iliyopita - dhidi ya Ubelgiji Machi mwaka huu na Bale aliridhishwa na matokeo hayo mjini Baku.

"Timu zote zilijitahidi kucheza. Mchezo uliokuwa mgumu kwa kiasi chache, lakini matokeo si mbaya na tumeyachukulia kwa mtazamo chanya," alisema Bale akiiambia BBC Sport.

"Tulitaka kushinda mchezo na tulikuwa na nafasi, lakini mambo yalikuwa tofauti na pointi moja si haba.

"Wakati unapokuwa nyuma kwa bao 1-0, unaweza kuwa na wakati tofauti na tulipambana kweli na tukafanikiwa kusawazisha.

"Tulicheza kwa kujituma na kwa nguvu zote. Ni ngumu kwa joto la sasa. Lakini najivunia wachezaji wenzangu. Baada ya mchezo tulisema tunatakiwa kutumia nafasi hii kwenye mchezo unaofuata."



## CASTAGNE AIPA PIGO UBELGIJI EURO 2020

**ST PETERSBURG, Russia**

MLINZI wa pembeni wa Ubelgiji, Timothy Castagne, atakosa kwa kipindi chote kilichobaki cha michuano ya Euro 2020 baada ya kuvunjika mfupa wa mfuko wa jicho.

Kikosi cha Roberto Martinez, Ubelgiji kilifungua mchezo wake wa kwanza wa Euro 2020 kwa ushindi mzuri wa mabao 3-0 dhidi ya Russia Jumamosi.

Castagne na Daler Kuzyaev wa Russia waligongana vichwa katika dakika ya 25 na wote walidondoka.

Haraka Castagne alitolewa na Kuzyaev dakika mbili baadaye kwenye mchezo huo wa Kundi B hapa St Petersburg.

"Kwa uhakika ni habari mbaya, habari mbaya kuondoka Timothy Castagne atakuwa nje ya mashindano haya," alisema kocha Mkuu wa Ubelgiji, Martinez.

"Alifanyiwa vipimo, na inaonyesha amevunjika mara mbili kwenye mfupa wa jicho na sasa yupo kwenye matibabu."

Wakati nyota huyo wa klabu ya Leicester City, Castagne atakuwa nje kwa kipindi chote cha mashindano hayo, habari njema ni kuhusu Jan Vertonghen.

Mlinzi mkongwe Vertonghen alitolewa dakika ya 77 kutokana na kuumia, lakini Martinez amesema hali yake inaendelea vizuri

"Vertonghen alipata maumivu kidogo, aliumia kifundo cha mguu na atasubiri kwa saa 48 kuangalia maendeleo yake, lakini hatutarajii kwamba, atakuwa ameuamia sana," aliongeza Martinez.

# DONDOO Z KA
## MAGAZETI Y YA




# WIJNALDUM AFUNGUKA SABABU KUITOSA BARCA

## ●●● Hatukuweza kufikia makubaliano, na PSG walikuwa haraka sana wakafanya kweli...

**AMSTERDAM,** Uholanzi

GEORGINIO Wijnaldum ameelezea kujiunga kwake na Paris Saint-Germain kwa sababu "walikuwa haraka kwenye maamuzi" baada ya mazungumzo na Barcelona kusimama.

**Mkataba wa Wijnaldum na Liverpool unamalizika mwishoni mwa msimu huu na sasa kituo chake kinachofuata kimethibitishwa kuwa ni PSG.**

Lakini nahodha huyo wa Uholanzi, ambaye aliiongoza timu yake kwa mabao nane wakati wa kufuzu Euro 2020, alitarajiwa kujiunga na kocha wake wa zamani wa 'The Oranje', Ronald Koeman pale Barca baada ya wiki za uvumi, lakini hakuwa na dili lolote lililofikiwa na kuwaruhusu PSG kumsajili haraka.

Wijnaldum alisema jana akiwaambia waandishi wa habari: "Nilifanya majadiliana na Barcelona kwa wiki nne na bahati mbaya hatukufikia makubaliano.

"Paris Saint-Germain walikuwa na haraka na wakafanya maamuzi. Na dili walilonipa ni kubwa sana kwa upande wangu.

"Lilikuwa chaguo gumu. Naweza kusema kwamba, mimi mwenyewe nilifikiria kwamba ningekwenda Barcelona, pia kwa sababu Barcelona ilikuwa ndio klabu pekee iliyokuwa inanihitaji sana mimi kwa wakati huu.

"Lakini hatukuweza kufikia makubaliano, na PSG wakafanya kweli."

Wijnaldum anaondoka baada ya kucheza mechi 235 kwa Liverpool kwa kipindi cha miaka mitano, akifunga mabao 22 na kutoa pasi za mwisho 15, lakini sasa akili yake ipo kwenye michuano hii ya Euro.

Jana Jumapili Uholanzi ilikuwa ikicheza na Ukraine kwenye mchezo wake wa kwanza wa michuano hiyo.

## ZISIKUPITE

### MARCELO AWANIWA EPL

EVERTON na Leeds United zote zinawania kumsajili mlinzi wa pembeni wa Real Madrid, Marcelo, wakati huu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 raia wa Brazil, akiwa hayupo kwenye mipango ya kocha mpya wa Real, Carlo Ancelotti. ***(Sunday Mirror)***

### VIEIRA NA UKOCHA B'MOUTH

KLABU ya Bournemouth imefanya jaribio jingine la kumtaka gwiji wa Arsenal, Patrick Vieira, kuwa kocha wao mpya, baada ya kujaribu kumshawishi mchezaji huyo wa zamani wa timu ya Ufaransa mwenye umri wa miaka 44, Februari mwaka huu. ***(Sunday Mirror)***

### GONZALEZ AGOMBEWA

TOTTENHAM inapambana na Fiorentina kuwania saini ya mshambuliaji wa Stuttgart na Argentina mwenye umri wa miaka 23, Nico Gonzalez. ***(Sky Italia)***

### UNITED BADO NA SANCHO

MANCHESTER United bado wanamwania nyota wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21 baada ya ofa ya kwanza kugonga mwamba kule Borussia Dortmund wiki iliyopita. ***(Sunday Times)***

### ARSENAL YAMTAKA DE BEEK

ARSENAL imefanya mawasiliano na Manchester United kuhusu nia ya kutaka kumsajili kiungo wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 24. ***(90min)***

### DEMBELE APEWA CHAGUO

BARCELONA itamwambia winga wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24, achague moja kusaini mkataba mpya au kuondoka klabuni hapo. ***(ESPN)***

### TRIPPIER KUUZWA PAUNI MIL. 30

ATLETICO Madrid imeweka mezani wazi kuwa Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30, atauzwa kwa pauni milioni 30. Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amekuwa akitajwa kumwania mlinzi huyo wa kulia. ***(Sunday Mirror)***

### MARTIAL AWEKWA SOKONI

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amemweka sokoni mshambuliaji wa Ufaransa, Anthony Martial, 25, huku Real Madrid wakihusishwa na straika huyo. ***(Sunday Express)***

### LUKAKU HAITAKI CHELSEA

STRAIKA wa Ubelgiji, Romeu Lukaku amekanusha uvumi kwamba anaweza kurudi katika klabu yake ya zamani ya Chelsea kipindi hiki cha majira ya joto, kwani ana furaha hapo Inter Milan. ***(HLN, via Mail on Sunday)***

### LEICESTER WAMTAKA PATSON

LEICESTER City imeungana na Liverpool, Chelsea na Tottenham katika mbio za kumwania straika wa RB Salzburg na Zambia, Patson Daka mwenye umri wa miaka 22. ***(Sunday Express)***

HABARI MICHEZO

## Daraja la Kwanza Zanzibar Juni 21

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), kupitia bodi ya ligi, limesogeza mbele michezo ya Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja iliyopangwa kuchezwa leo kwa mujibu wa ratiba ya awali.

Michezo hiyo sasa imepangwa kuchezwa Jumatatu ya Juni 21, mwaka huu na itafunga rasmi pazia la ligi hiyo msimu huu kwa kupatikana timu itakayopanda daraja kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili Makamu Mwenyekiti wa Bodi Ligi, Sheha Mohammed, alisema kusogezwa mbele kwa michezo hiyo ni kutokana na kusubiri kusikilizwa malalamiko mawili yaliyopo mezani mwa kamati hiyo kati ya timu ya Mwembe Makumbi City dhidi ya Gulioni FC na New King dhidi ya Ngome FC.

"Michezo iliyopangwa kuchezwa kesho ndiyo itakayotoa majibu kwa timu itakayopanda daraja na zile mbili zitakazoshuka, hivyo kama bodi ya ligi, tumeona tusogeze mbele ili tuipe muda kamati ya kusikiliza malalamiko yaliyopo mezani mwao na kutoa majibu kabla ya hizi mechi kuchezwa," alisema.

## Jang'ombe, New King kutifuana FA Cup leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MICHUANO ya Kombe la Shirikisho Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup, kwa hatua ya 16-bora inatarajiwa kuendelea kutimua vumbi leo kwa kupigwa mchezo mmoja katika Uwanja wa Amaan.

Mchezo huo utazikutanisha New King na timu ya Taifa Jang'ombe, zote kutokea Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Mashindano hayo hayo, Haji Issa "Kidali", alisema michuano hiyo awali ilisimama ili kupisha kumalizika kwa Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema ratiba ya Ligi Kuu Zanzibar ilibana na kushindwa kupatikana nafasi ya kuendelea kwa michuano hiyo huku pia kukichangia na suala zima la uhaba wa viwanja.

Hata hivyo, alizitaka timu ambazo zimesonga mbele katika michuano hiyo hususan zile za madaraja ya chini, kufuata kanuni za mashindano ili kuweza kumaliza michuano hiyo kwa wakati.

# MOROCCO APIGIA HESABU POINTI 12 NAMUNGO FC

**Na Saada Akida**

MECHI nne zilizobaki kabla ya kuhitimisha msimu wa Ligi Kuu Bara, zimegeuka kaa la moto kwa Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, baada ya kueleza zinampa wakati mgumu hadi kutofikiria suala la usajili kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu ujao.

**Kauli hiyo ya Morocco inakuja kutokana na baadhi ya makocha wa timu za Ligi Kuu kukabidhi ripoti zao mapema kwa uongozi kwa ajili ya mapendekezo ya usajili wa msimu mpya.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Morocco alisema kutokana na mechi ngumu zilizopo mbele yao na kuhitaji kupata pointi ili kumaliza katika nafasi nzuri kwenye ligi hiyo, kunamfanya achelewe kukabidhi ripoti hiyo, hivyo kusubiri hadi mwishoni mwa msimu.

Alisema kwa sasa kikosi chake kipo Musoma tayari kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya Biashara United utakaopigwa kesho, Jumanne.

"Tumeshafika Musoma kwa ajili ya mechi yetu dhidi ya Biashara United, ni mechi ngumu na ya ushindani mkubwa, ila tumejipanga kuhakikisha tunafikia malengo yetu ya kumaliza tukiwa katika nafasi ya nne za juu katika msimamo.

"Kwa sasa nina pointi 41, ili nimalize nafasi nne za juu lazima nishinde mechi zote hizo, tunahitaji kupambana hali ambayo akili na nguvu kuelekeza katika malengo hayo, suala la usajili litakuwapo baada ya kumaliza msimu," alisema Morocco.

Alisema wanapambana kutafuta pointi tatu katika mchezo huo baada ya hapo watarejea jijini kucheza dhidi ya Azam FC, Ruvu Shooting pamoja na Simba mechi ambazo zote ni ngumu kwao.

Namungo iko nafasi ya nane ikiwa na pointi 41 na imebakiza mechi dhidi ya Biashara United, Azam FC, Ruvu Shooting na Simba, na endapo ikishinda zote itakuwa imekusanya pointi 53.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot, Juma Kambwi, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 11.2 baada ya kukabidhiwa mwishoni mwa wiki kutokana na kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa ambayo kwa sasa dau limefika Sh. milioni 314. 9. **PICHA: SPORTPESA**

# Yanga kileleni Ligi ya Vijana U-20

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa mabao 2-0 juzi saa moja usiku katika Uwanja wa Azam Complex Chamazi, Dar es Salaam dhidi ya JKT Tanzania, timu ya Yanga chini ya miaka 20, imekwea kileleni mwa msimamo wa Kundi B kwenye Ligi ya Vijana chini ya umri huo inayoendelea nchini.

Kikosi cha Yanga kinachonolewa na winga wa zamani wa timu hiyo, Said Maulidi, kiliwaadhibu maafande wa JKT Tanzania mabao 2-0, yaliyowekwa wavuni na Yohana Ndushi dakika ya 55 na Abby Mikimba dakika ya 77 na kuifanya timu hiyo kuongoza Kundi A kwa tofauti ya mabao.

Wakati Yanga ikishinda, watani zao wa jadi, Simba nao majira ya saa tatu usiku waliichapa Mwadui bao 1-0 na kuwafanya kuwa na pointi nne sawa na Yanga, lakini ikizidiwa kwa tofauti ya bao moja.

Ikumbukwe kuwa kwenye mechi ya ufunguzi Alhamisi iliyopita, Simba na Yanga zilitoka sare ya bila kufungana na kugawana pointi moja moja.

JKT Tanzania inafuatia ikiwa na pointi tatu na inayoshika mkia ni Mwadui FC ambayo haina pointi, baada ya kufungwa mechi mbili dhidi ya JKT Tanzania na Simba.

Kundi B lina timu za Azam FC, Mtibwa Sugar, Prisons na Kagera Sugar.

Kila kundi litatoa washindi wawili watakaoshika nafasi mbili za juu na kucheza nusu fainali na zitakazoshinda, zitapambana kwenye fainali kupata bingwa wa Ligi ya Vijana chini ya miaka 20 msimu huu.

Michezo
Jumatatu Juni 14, 2021
Nipashe



Wijnaldum afunguka kuitosa Barca UKURASA 22

PAMOJA BONANZA...



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akifanya mazoezi ya viungo katika bonanza la CRDB Bank Pamoja, baada ya mbio fupi zilizoanzia viwanja vya Bunge. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto) na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (kulia). **NA MPIGAPICHA WETU**

# Stars yaanza kunoga

## Yatandaza soka biriani na kuichabanga Malawi iliyopo juu katika viwango vya Fifa...

**Na Adam Fungamwango**

WINGA Kibu Denis anayechezea klabu ya Mbeya City ambaye aliingia kipindi cha pili, jana alibadilisha sura ya mchezo na kuwa chachu ya ushindi wa mabao 2-0 kwa Taifa Stars dhidi ya timu ya Taifa ya Malawi, The Flames.

**Ulikuwa ni mchezo wa kirafiki ulio kwenye Kalenda ya FIFA, ukipigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Nahodha John Bocco aliifungia Stars bao la kwanza dakika ya 68 baada ya kupata pasi tamu kutoka kwa Kibu ambaye alikuwa amemnyang'anya beki mmoja wa Malawi mpira karibu na eneo la hatari, kabla ya kuvuta hatua tatu na kutoa pasi murua kwa mfungaji.

Mchezaji huyo aliyeingia badala ya Salum Aboubakar 'Sure Boy', aliangushwa nje kidogo ya eneo la hatari dakika sita baadaye na kuwa faulo ambayo ilipigwa na Israel Patrick Mwenda na kuujaza wavuni na kumuacha kipa Brighton Muntali akishangaa.

Mpira ulianza kwa kasi na kwenye sekunde ya 30 tu, nahodha Bocco alimiminiwa krosi kutoka kwa Shomari Kapombe, lakini akapiga kichwa mpira ukatoka juu ya lango la Malawi ambayo katika viwango vya ubora vinavyotolewa na Fifa ipo nafasi ya 115 kwa mwezi uliopita huku Tanzania ikiwa nafasi ya 137.

Yusuph Mhilu naye alikosa bao la wazi dakika ya tano, akipiga mpira nje ya lango baada ya kubaki na kipa wa Malawi, Muntali. Taifa Stars iliendelea kutawala kabumbu, huku Malawi ikionekana kusoma mchezo na ilianza shambulio la kwanza dakika ya 22.

Alikuwa ni mchezaji anyecheza soka la kulipwa nchini Urusi kwenye klabu ya Sheriff Tiraspol, Peter Banda, alipoupata mpira uliookolewa na mabeki wa Stars akiwa nje kidogo ya eneo la hatari, akapiga shuti la kiufundi, lakini ukitoka juu kidogo ya lango. Mchezaji huyo anacheza timu hiyo kwa mkopo akitokea Big Bullets FC ya nchini Malawi.

Aishi Manula aliiokoa Stars kufungwa dakika ya 38 alipopangua shuti kali la mbali na kuwa kona tasa.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, Stars ikiwatoa Erasto Nyoni, Sure Boy, Shomari Kapombe, Yusuph Mhilu, Nickson Kibabage na Mudathir Yahaya na nafasi zao kuchukuliwa na Kennedy Juma, Kibu, Ayoub Lyanga, Mwenda, Mzamiru Yassin na Abdul Selemani, mabadiliko ambayo yaliisaidia sana Stars chini ya Kocha Mkuu Kim Poulsen.

# Mkwasa apigia hesabu tatu za Yanga Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Mkwassa (pichani chini), amesema tayari kikosi chake kimerejea kambini na kuanza mazoezi kwa ajili ya kuivutia kasi Yanga katika mchezo wao ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti wiki iliyopita, Mkwassa alisema hawako katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo, hivyo analazimika kuiandaa timu yake vizuri kwa ajili ya kutafuta pointi tatu katika kila mechi iliyopo mbele yao ikiwamo dhidi ya Yanga watakayocheza Alhamisi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Alisema anaamini utakuwa mchezo mgumu na wa ushindani mkubwa kwa sababu kila timu inahitaji kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo.

"Mechi nyingi hivi karibuni hatukufanya vizuri, sasa tunajipanga kuanza na dhidi ya Yanga, Polisi Tanzania na Namungo FC, hizo tunahitaji kupata pointi ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kubaki katika Ligi Kuu.

"Kwa sasa hakuna kubeza timu yoyote, tutakosa baadhi ya wachezaji kuelekea mchezo wetu dhidi ya Yanga, kutokana na kutumikia adhabu ya kadi na majeruhi, lakini tayari nimewaandaa vijana wangu kuhakikisha wanapambana kufikia malengo yetu," alisema Mkwassa ambaye timu yake inashika nafasi ya 10 ikiwa na pointi 37.

9 770856 541002 >